epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Oktoba 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581837
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

RIPOTI YA UCHUNGUZI -2
MIKOPO MTANDAONI

# Wakopaji wasimulia madhila ya kutisha




• **Mbunge** adokeza 65 wamejiua kwa kujinyonga na kunywa sumu katika mikoa minane nchini... *Endelea ukurasa 4*

UKURASA WA 3

## DK. MPANGO ALIA NA 'MASHANGAZI', ATAKA UTAFITI SOKO LA AJIRA KWA VIJANA



UKURASA WA 3

## UBIA WA TEKNOLOJIA CHINA NA TANZANIA KUPAFANYA NCHINI KUWE KITOVU CHA HABARI MTANDAONI



UKURASA WA 19

## GACHAGUA AMTUPIA LAWAMA RAIS RUTO, AKILALAMIKA UHAI WAKE UKO SHAKANI



## Waziri: Polisi hakikisheni usalama wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

UKURASA 2



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiangalia matokeo ya utafiti mbalimbali yaliyotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF) jijini Dar es Salaam kabla ya kufungua Mkutano wa Kusherehekea Miaka 30 ya taasisi hiyo jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, Prof. Fortunata Makene. **PICHA: OMR**




# Polisi yafunguka kisa na mkasa kuwashikilia makada CHADEMA

UK. 2

**MICHEZO** GAMONDI AIHOFIA JKT, FADLU ATAKA VAR UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Ujumbe wa Umoja wa Mabalozi mbalimbali wa nchi za Bara la Afrika, ukiongozwa na Mwenyekiti wake, Balozi wa Comoro nchini, Dk. Ahamada El Badaoui Mohammed (kulia kwa Rais), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Polisi yafunguka kisa na mkasa kuwashikilia makada CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi limeeleza sababu ya kuwashilikia makada wawili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kuwa ni madai ya kuvamia vituo vya kuandikisha wananchi katika Daftari la Wakazi na kufanya fujo.

Taarifa iliyotolewa juzi na Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Masime, ilieleza kuwa Mwenyekiti wa Jimbo la Iringa, Frank Nyalusi alikamatwa Oktoba 20, 2024 huko Iringa baada ya kutembelea vituo vya kuandikisha wananchi katika Daftari la Wakazi na kulazimisha apewe madaftari hayo.

Kupitia taarifa hiyo, DCP Misime alisema kuwa kabla ya kukamatwa, alipigiwa simu na Jeshi la Polisi ili ajisalimishe kituoni, lakini alikaidi ndipo ikawalazimu askari polisi kwenda kumkamata.

Alisema taarifa zilizosambazwa katika mitandao ya kijamii kuwa kiongozi huyo alipigwa na polisi baada ya kukamatwa si za kweli na kuwataka watanzania kuzipuuza.

"Jeshi la Polisi lingependa kusema suala la kupigwa halipo na aliyeandika hivyo ni kutaka kutia chumvi, ili apate wafuasi wa kushabikia uongo wake," alidai DCP Masime.

Alisema jeshi hilo pia lilimkamata Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Katavi, Rhoda Kunchela na wenzake Oktoba 19 mwaka huu baada ya kupokea taarifa kuwa walimvamia karani wa uandikishaji wapigakura katika kijiji cha Songambele, wilayani Mlele, mkoani Katavi, kumfanyia fujo na kumnyang'anya daftari alilokuwa anaandikisha wapigakura.

DCP Misime alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, polisi walianza uchunguzi kwa kupata maelezo ya aliyefanyiwa uhalifu huo na mashahidi wengine, kisha waliwafuatilia na kuwakuta wamejifungia katika nyumba na kufanikiwa kuwakamata na kuwafikisha kituoni kwa hatua zingine za kisheria.

Aliwataja wengine waliokamatwa kuwa ni Festo Mgombele, Juma Masoud, Melkio Melkiades, Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Katavi, Meshack Konja na Nsajigwa John.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa onyo kwa watu ambao wanafika vituo vya uandikishaji wapigakura kwa nia ya kufanya uhalifu kuwa watakamatwa na hatua za kisheria zitafuatwa, ikiwamo kufikishwa mahakamani.

### LHRC YALAANI

Kukiwa na angalizo hilo la polisi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimelaani vikali kutekwa, kudhalilishwa na kupigwa kwa Katibu Mwenezi wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) Taifa, Aisha Machano, kikisisitiza kuwa ni kinyume na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Dk. Anna Henga alisema wanalaani vikali vitendo hivyo ambavyo vinaendelea katika kipindi hiki cha mchakato wa uchaguzi.

Dk. Anna alisema LHRC inavitaka vyombo vya dola kuwasaka watuhumiwa popote walipo, kuwatia mbaroni na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria ili hatua stahiki zichukuliwe.

"Tunataka vyombo vinavyohusika kufuata sheria pindi vinapomkamata mhusika au wahusika wa uhalifu, afikishwe mahakamani ndani ya muda husika uliotolewa kisheria," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa hivi karibuni kumekuwa na matukio yanayojirudia yanayokwenda kinyume cha haki za binadamu katika maeneo tofauti nchini, jambo ambalo alisisitiza hawatalifumbia macho.

Alisema kuwa jana Oktoba 21 ni Siku ya Haki za Binadamu Afrika na inasikitisha kuona Tanzania inaadhimisha siku hiyo kukiwa na matukio mengi ya viashiria vya uvunjifu wa haki za binadamu, yakijumuisha kukamatwa baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa.

"Vitendo vya kunyanyasa na kuumiza wanawake, hususani wanaojihusisha na siasa katika kipindi hiki cha uchaguzi, hakikubaliki hata kidogo kwani ni kinyume cha sheria na haki za binadamu," alionya.

***Imeandikwa na Jenifer Gilla na Pilly Kigome**


## SINCRO SITEWATCH LIMITED
### DAR ES SALAAM TANZANIA

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Sincro Sitewatch Limited** watauza kwa mnada wa hadhara Magari 13 tarehe 26 Octoba, 2024 Jumamosi kuanzia saa 5:00 asubuhi. Mnada utafanyika Ofisi za SINCRO iliyopo kwenye Kitalu 1337 Mtaa wa Msonge Mikocheni A nyuma ya Mgahawa wa Golden Fork uliopo Mikocheni

**Magari yatakayouzwa.**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser Pick Up | 1HZ Petrol Engine | 2000 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Hilux Double Cabin | 2KD Diesel Engine | 2006 | Umelipwa |
| 2 | Nissan Pick Up Single Cabin | ZD30 Diesel Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado S. Wagon | 1KZ Diesel Engine | 1994 | Umelipwa |
| 4 | Toyota RAV4 Station Wagon | 3S,1AZ,1ZZ,Petrol Engine | 1995,2000, 2002,2005 | Umelipwa |
| 1 | Ford Ranger Double Cabin | AF Diesel Engine | 2007 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Grande Mark II Saloon | 1G Petrol Engine | 2001 | Umelipwa |
| 1 | Suzuki Carry Pick Up | F6 Petrol Engine | 1998 | Umelipwa |
| 1 | Bedford Truck TM 4X4 (Four Wheel Drive) | SKF Diesel Engine | 1992 | Umelipwa |

Magari yote yataweza kukaguliwa kwenye offisi za Sincro Sitewatch Limited, zilizopo litalu 1337, Mtaa wa Msonge Mikocheni A nyuma ya Mgahawa wa Golden Fork Mikocheni kuanzia tarehe 23 mpaka 25 Octoba 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 1 Novemba, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB yanakubalika.**
3. Magari yote yatauzwa kama yalivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa kodi zote za kuhamisha umiliki.
5. Magari yote yaliyouzwa yataondolewa baada ya kuhamisha umiliki.
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926 E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**


## Waziri: Polisi hakikisheni usalama katika Uchaguzi Mitaa

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amevitaka vyombo vya dola nchini, likiwamo Jeshi la Polisi, kuhakikisha vinaimarisha usalama, ili Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uwe wa huru na haki.

Ameelekeza umewekwa utaratibu maalumu wa kuzuia udanganyifu katika uchaguzi, ikiwamo mpigakura mmoja kupiga zaidi ya mara moja katika vituo tofauti, akisisitiza watatumia mifumo ya kiusalama kubaini.

Mchengerwa aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam alipofunga uandikishaji wapigakura katika Daftari la Makazi, zoezi lililoendeshwa kwa siku 10 kufikia juzi.

Alisema kuwa baada ya kumaliza hatua hiyo, kuanzia jana mpaka Oktoba 27 mwaka huu, orodha ya wapigakura itabandikwa katika sehemu za matangazo ya uchaguzi ili kuwawezesha wananchi wahakiki majina yao.

Waziri huyo alisema hatua hiyo itawapa fursa wananchi ama kurekebisha majina yao, kubadili taarifa au kufuta jina iwapo aliyeorodheshwa amefariki dunia huku akiwataka waliojiandikisha kufika kuhakiki.

Pia aliwataka wananchi wenye sifa za kuchaguliwa kuwa viongozi, wajitokeze kuanzia Oktoba 26 mpaka Novemba Mosi kutimiza haki yao ya kikatiba kugombea nafasi za uongozi.

Mchengerwa alibainisha kuwa jumla ya wapigakura 31,282,331 wamejiandikisha sawa na asilimia 94.83 ya lengo la kuandikisha watu 32,897,8579. Kati yao, wananume ni 15,236,772 sawa na asilimia 48.71 na wanawake ni 16,045,559 sawa na asilimia 51.29.

Baadhi ya maeneo mkoani Mwanza, ikiwamo mitaa ya Iseni, Hospitali pamoja na Aman, yote ya kata ya Butimba, wilayani Nyamagana, majina yalichanwa asubuhi kabla ya uhakiki kuanza.

Katibu wa CHADEMA, Kata ya Butimba, Athelius Audax, alisema licha ya majina hayo kuchanwa katika maeneo mengine, ukiwamo mtaa wa Kanyerere, wamebaini ongezeko la majina tofauti na yale yaliyoshuhudiwa na mawakala wao juzi jioni.

**Imeandikwa na Halfani Chusi (DAR) na Vitus Audax (MWANZA)**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email:*
**customerrelations@guardian.co.tz**

HABARI KITAIFA

# Mpango ataka utafiti zaidi soko la ajira

**Na Faustine Feliciane**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF) kujikita kwenye utafiti wa maeneo ya soko la ajira na namna vijana wanavyoweza kuendana na soko hilo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa kongamano la kitaifa ya kuadhimisha miaka 30 tangu kuanzishwa kwa ESRF, alisema Tanzania kama zilivyo nchi nyingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara, haijafanikiwa kufikia matunda ya ongezeko la watu wanaofanya kazi.

Alisema wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya ufundi wanaoweza kufanya kazi ni kati ya 800,000 hadi 1,000,000.

"Hata hivyo, kwa wastani nafasi za kazi zinazopatikana ni kati ya 30,000 hadi 90,000 katika sekta ya umma na binafsi, hii inaonyesha ubora wa wahitimu hauendani na ujuzi unaohitajika katika soko rasmi la ajira," alisema Dk. Mpango.

Alisema kwa sasa kumekuwa na tamaduni mbaya kwa baadhi ya vijana kujiingiza kwenye makundi ya kushinda vijiweni na wengine kwenye mahusiano na watu wenye umri mkubwa.



"Vijana wa kiume katika kutafuta wepesi wa maisha wamekuwa wajiingiza kwenye mahusiano na wanawake waliowazidi umri, maarufu wanaitwa 'mashangazi' au kujiingiza kwenye kucheza kamali," alisema Dk. Mpango.

Aidha, alisema serikali itaendelea kushirikiana na Taasisi ya ESRF na nyingine katika kufanya utafiti utakaolisaidia taifa katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

"Serikali inatambua juhudi za ESRF katika kuchochea maendeleo na kukuza uchumi wa taifa letu," alisema Dk. Mpango.

Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, Fortunata Makene, alisema wameyapokea maagizo ya Makamu wa Rais ya kufanya utafiti katika maeneo sita likiwamo eneo la soko la ajira na namna vijana wanavyonufaika nalo.

"Tutaendelea kushirikiana na wadau wetu, serikali na vyuo vikuu mbalimbali vya ndani na nje ya nchi ili kusaidia kuwajengea uwezo wataalamu wetu kwenye kufanya utafiti wenye tija kwa taifa," alisema Fortunata.

Alisema taasisi hiyo inajivunia katika ushiriki wake kwenye mipango ya serikali ya maendeleo na kukuza uchumi wa nchi.

## EATV wazindua msimu mpya wa mamalishe

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha East Africa Television (EATV) na East Africa Radio kimezindua msimu wa tano wa shindano la mamalishe unaolenga kuwaongezea thamani na kuwainua katika biashara zao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo mkoani Dar es Salaam jana, Mwakilishi wa EATV, Yusta Msowoya alisema shindano hilo linalofanyika kwa mara ya tano, linawashindanisha wafanyabiashara wadogo wa chakula Dar es Salaam na washindi wanapatiwa zawadi mbalimbali kutoka kwa wadhamini.

Aliwataja wadhamini wao kuwa ni Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Airtel, Mwendapole Real Estate, Kilimanjaro Institute of Technology Management, duka la vifaa vya umeme la Jaden na kampuni ya Eco Africa.

Alisema tangu kuanzishwa kwa kampeni hiyo idadi ya mamalishe iliyowafikia imeongezeka kutoka saba mwaka 2020 hadi 1,500 katika msimu wa nne uliofanyika mwaka jana na washindi walijipatia zawadi mbalimbali vikiwamo viwanja na mafunzo ya kuongeza thamani biashara zao.

Alisema kuwa katika msimu wa tano mwaka huu wanatarajia kuwafikia wafanyabiashara kati ya 3,000 na 5,000 ambapo mamalishe 10 kutoka wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam watachuana kwa mapishi ya vifungua kinywa kama vile maandazi, chapati, kalimati na donati.

"Msimu huu utaanza Oktoba 30, 2024 katika wilaya ya Kinondoni katika pishi la maandazi, kisha tutaelekea wilaya za Temeke, Ilala na Ubungo kutafuta mamalishe 10 watakaoshindana katika fainali," alisema.

Meneja wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Jackson Mbando, alisema wamevutiwa kushiriki katika kampeni hiyo kwa sababu inagusa moja kwa moja jamii ya watu wenye kipato cha chini.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha kuwa kupitia kampeni hiyo wanaboresha mazingira ya kazi ya kundi hilo kwa kuwapatia laini za Airtel na kuwaunganisha na huduma ya lipa namba ambayo itawawezesha kufanya malipo ya biashara zao bure.



Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu (kulia), akiteta jambo na Askofu Dk. Fredrick Shoo, Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, wakati wa harambee ya ujenzi wa kanisa, Usharika wa Naibili, Siha, Kilimanjaro. Tukio hilo lilifanyika Jumapili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## China kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha kidijiti

**Na Maulid Mmbaga**

CHINA inatarajia kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha kidijitali katika mawasiliano baada ya mataifa hayo mawili kuingia mkataba wa ushirikiano katika sekta hiyo.

Lengo ni kuchochea uchumi na kuongeza ufanisi wa teknolojia ya mawasiliano.

Jana Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilisaini mkataba wa ushirikiano na Kampuni ya Teknolojia ya Mawasiliano ya China (CECIS) ukilenga kuongeza ufanisi katika usalama wa mtandaoni nchini.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam wakati wa hafla ya kusaini makubaliano hayo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi, alisema mkataba huo pia utasaidia kutoa mafunzo kwa Watanzania kuhusu masuala mbalimbali ya usalama wa mtandaoni.

Alisema mkataba huo pia utasaidia vijana wa Kitanzania kwa ujumla kuwa na uwezo wa kufungua viwanda vyao wenyewe vitakavyotumika katika kutengeneza vifaa mbalimbali vya kielektroniki vinavyotumika katika mawasiliano kama mfano WiFi.

"Haya yote ni matokeo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya nchini China, ambako moja ya kampuni alizozifikia ni hii tunayoenda kushirikiana nayo, sisi kama wizara tunajivunia na wataalamu wetu kwa kuwa tumehakikisha tunafanya haraka katika mawasiliano ili hawa wenzetu waje kwa wakati.

"Lengo ni kuona kwamba tunakwenda kuzikamata zile fursa kwa haraka sana, na tunajenga 'habs' vituo vya TEHAMA nane katika nchi hii tayari fedha zimetoka, kazi zimeanza, na tunauhakika ujuzi walionao hawa wenzetu utaenda kutumika katika majengo hayo kuhakikisha tunaendelea kiteknolojia," alisema Maryprisca.

Aidha, aliongeza kuwa vijana watanufaika moja kwa moja kwa kupata elimu kutoka kwa wabobezi wa masuala ya usalama wa mtandaoni,

"Tunataka wafike mbali zaidi kwa kutuletea viwanda vinavyotengeneza vifaa ili ifike wakati kusiwe na haja tenda ya kuagiza vifaa vya mawasiliano nje pale taifa litakapokuwa na uhitaji," alifafanua.

Aidha, alieleza kuwa wanatamani ifike mahali badala ya kuagiza kompyuta, simu na televisheni nje, wanahitaji kuwe kunaletwa malighafi ili vifaa hivyo viundiwe hapa hapa nchini.

"Tunahitaji kuona pia tunakuwa na wataalamu wetu wa ndani, kwa hiyo pamoja na kwenda kuwatumia wataalamu hawa kutoka China, lakini pia tunawatengeneza vijana wetu kubobea katika sekta hiyo, na Rais Samia alipokuwa kule walikubaliana maeneo kumi ya kuja kuyashughulikia mojawapo ni hili la TEHAMA," alisema Maryprisca.

Mwenyekiti wa Kampuni hiyo ya CECIS, Guo Zhaoping, alisema anaimani kwa ushirikiano huo utasaidia kuleta mafanikio katika pande zote mbili, kuinua na kuongeza ufanisi na kuwa na mafanikio ya muda mrefu katika sekta ya mawasiliano.

Alisema walifanya mazungumzo na makatibu wa Rais Samia jinsi ya kuimarisha ushirikiano kati ya pande hizo mbili. Na chini ya uungwaji mkono kutoka kwa serikali ya zote mbili, hatimaye walifikia makubaliano hayo.

"Ushirikiano wetu umejikita katika kuendeleza matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika uboreshaji wa mfumo wa utawala wa kitaifa na uwezo wake wa kisasa, hasa katika kuunga mkono maendeleo ya haraka ya uchumi wa kidijitali, kampuni yatu itakuwa na jukumu muhimu katika ushirikiano huu.

"Kuunda mradi wa kielelezo katika uwanja wa ushirikiano unaotegemea uaminifu kutaweka kigezo cha ushirikiano wa siku zijazo na kusaidia kupanua matumizi ya teknolojia za kidijitali, hasa katika maeneo ya utawala na uchumi," alisema Zhaoping.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

## RIPOTI YA UCHUNGUZI -2

MIKOPO MTANDAONI

# Wakopaji wasimulia madhila ya kutisha

• Mbunge adokeza 65 wamejiua mikoa minane

**Na Mwandishi Wetu**

***Sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana iliangazia orodha ya kasoro za utoaji mikopo ya mtandaoni, huku Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ikitoa mwongozo kuhusu uendeshaji huo wiki kadhaa baada ya mwandishi wa gazeti hili kutaka kupata ufafanuzi wake.***

***Vilevile, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ukaweka bayana hauwatambui wakopeshaji hao. Endelea na sehemu ya pili yenye undani wa madhila yaliyomo katika makubaliano ya mikopo hiyo...***

MMOJA wa waathirika wa mikopo hiyo, Jackline Meena, anasema alikopa Sh. 50,000 lakini alilipa Sh. 250,000 na waliendelea kumdai na alipogoma kulipa waliunda kundi la WhatsApp kisha wakaweka picha yake na kuwaunga watu wote waliohifadhiwa katika simu yake, wakimdhalilisha kuwa amewatapeli fedha.

"Niliripoti polisi na nilitumia mbinu zangu kuwapeleka polisi hadi kwenye ofisi waliyokuwapo ambayo haikuwa inajihusisha na masuala ya mikopo. Polisi walikamata wafanyakazi wote hadi meneja rasilimali watu ambao walibaini kuwa watu hao ni wa Mkopo Fasta, App inayomilikiwa na raia wa China.

"Watu wamefukuzwa kazi, watu wameharibiwa ndoa zao kisa mikopo. Unachukua mkopo kwa njia ya mtandao labla Sh. 500,000 ndani ya siku saba.

"Siku mbili kabla ya kulipa wameshaanza kukutumia matusi. Wanaunda kundi la WhatsApp, wanaweka picha yako kisha wanaanza kuandika matusi," anasema askari polisi aliyeomba hifadhi ya jina lake. Ni miongoni mwa walioshiriki kumkamata Meneja Rasilimali Watu wa App ya Mkopo Fasta.

Anaendelea kueleza kuwa: "Kuna mama mmoja walimsambaza mtandaoni wakiandika: "Mimi Julian, ninauza..." halafu wakaunga namba za simu za watu walio katika simu yake.

"Wanaingia kwenye mawasiliano ya simu ya mkopaji kisha wanatumia taarifa zake kumdhalilisha. Tumekagua hadi BRELA hawatambuliki, ni kampuni za ujanjaujanja zinazoibia wananchi."

Askari polisi huyo anasema ufuatiliaji wao ulibaini walikuwa na ofisi Mwenge, wilayani Kinondoni, lakini baadaye walihamia Mikocheni (Kinondoni).

"Baadhi ya walioshtaki polisi, walirejeshewa fedha zao na fidia ya usumbufu kisha wakaamua kuachana na kesi," anasema askari huyo.

Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Felista Njau, anasema amefanya utafiti tangu mwaka 2020 na kukutana na kero hizo katika majimbo mbalimbali, wakopeshaji hao wanabadili majina ya taasisi zao kila mara, lakini lengo ni kutoa mikopo yenye riba kubwa. Walengwa wakuu ni wanawake.

"Wanawakopesha wanawake zaidi kwa kuwavutia kwa kuwaambia ni mikopo inatolewa ndani ya muda mfupi na watarejesha kwa urahisi.

"Wanawadanganya riba ni nafuu, wanawake wengi hawajui asilimia 10 ya Sh. 200,000 ni Sh. 20,000, hawawaambii ukweli, nimekuta kuna mikopo yenye riba kubwa mno.

"Kuna mama anakopa Sh. 50,000 lakini anarejesha hadi inafika Sh. 175,000, wanawadanganya kwa dhamana ndogo, wanawake wanadhalilishwa na kufilisiwa na wengine wameachika na kukimbilia mjini kwenda mafichoni baada ya mali zao kama friji, brenda na samani za nyumba kuchukuliwa," anasema.

Mbunge Felista anasema kuwa katika utafiti wake, amebaini wanawake 65 wamefariki dunia kwa kujinyonga au kunywa sumu katika mikoa minane nchini, huku wengine wakijidhuru na kuachika kutokana na madeni yasiyokwisha.

"Tumezalisha ombaomba, dadapoa (wanawake wanaofanya biashara ya ngono), wanajiuza ili wapate kuishi baada ya mtaji wao kudhulumiwa na wakopeshaji ambao wemeingia mtandaoni kuibia watu.

"Hali ni mbaya. Hiyo mikopo ya mitandaoni, wanaambiwa andika majina ya watu wawili unaowajua, akishatumiwa Sh. 50,000 ya mkopo baada ya siku mbili wale alioweka namba zao wanaanza kudaiwa. Akichelewa kulipa, picha inawekwa mtandaoni 'huyu ni mdaiwa sugu, ni malaya anajiuza' na udhalilishaji mwingine," Felista anasema.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba.

Mbunge huyo anaitaka BoT kuzifuatilia kwa karibu taasisi ndogo za fedha (microfinance) na kuchukua hatua kali kwa kuwa sheria zipo na hatua zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya udhalilishaji unaoendelea hivi sasa.

Katika uchunguzi wake, mwandishi wa habari hii amebaini ujumbe unaotumwa kwa watu wa karibu na mkopaji ni pamoja na unaosomeka, "Ndugu wa karibu, jamaa, rafiki, jirani wa... (jina la mkopaji na namba zake za simu) aliyechukua mkopo kwa njia ya mtandao kupitia App ya... (wanataja jina la mkopeshaji), unafahamishwa kuwa mtu huyu amekiuka makubaliano ya kutolipa deni siku husika ya marejesho na kutopokea simu za ofisi, hivyo tutamchukulia hatua kwa kosa hilo.

"Unaombwa kumpigia simu mhusika na kumjulisha kuwa ana saa mbili za kulipa deni kabla hatua kali hazijachuliwa dhidi yake. Fanya hivyo kuepuka usumbufu."

Ni ujumbe unaotumwa kwa watu wa karibu na mkopaji ukiwa na lengo la kuwataka wawe sehemu ya kumshinikiza mdaiwa kulipa deni lake.

Kitendo hicho ni ukiukwaji wa Kanuni za Ukusanyaji Madeni Toleo la Mwaka 2019 la Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Ibara ya 56 (1) (c) na (d).

Kanuni zinakataza kumtisha au kutumia nguvu au njia zisizo halali kukusanya au kufuatilia deni, pia kutotumia lugha inayofedhehesha au isiyofaa.

Rashidi Mazengo Mkazi wa Mbagala, anasema aliomba mkopo mtandaoni, aliambiwa anapaswa awe na namba ya kitambulisho cha uraia.

"Pia niliambiwa niwape namba za simu za watu wawili ambao watanidhamini na kisha baada ya kukamilisha utaratibu huo ningewekewa fedha.

"Walichukua namba za watu wangu wa karibu, wakaanza kuwatumia ujumbe mfupi kila mtu mwenye namba yangu, hii haijakaa sawa kwa sababu ni kuniaibisha," analalama.

Mkopaji mwingine Neema Mmegelwa, mkazi wa Mbagala Zakiem, anasema alikopa Sh. 40,000 zilizogeuka shubiri, hata akakimbia makazi yake.

"Kama ni ujumbe wa kukumbushwa kuwa ninadaiwa, nitumiwe mimi, siyo watu wenye namba yangu. Iweje leo nianze kutangazwa? Kwanini shida yake iwe tabu kwa watu wengine?

"Niliwahi kufuatwa mpaka nyumbani kwangu, ninaamka asubuhi, ninakuta gari lipo uwanjani wanataka fedha zao. Vitisho vingi, kila siku unatumiwa meseji inasema 'tunapeleka taarifa zako kwa Jeshi la Polisi', mara 'utajuta tutakachokufanyia', anasema Neema.

Jackson Mwalongo, dereva wa bodaboda mkoani Dar es Salaam, anasema kuwa wakati anakopa, hakujua kama wanatuma ujumbe kwa watu pindi anapochelewesha marejesho.

"Nimekopa Sh. 120,000, nililipa Sh. 50,000 nikapitiliza kulipa. Wakawa wanapiga simu, kila nikiwaelewesha hawanielewi, mwisho nikaamua kutopokea simu zao. Cha ajabu, ninapigiwa simu na watu tofauti kuwa ninadaiwa, tena wananitukana," anasema Mwalongo.

Zuhura Ramadhani, mkazi wa Magomeni, wilayani Kinondoni, anaonya watu kutoingia katika mifumo ya mikopo hiyo hata kama wana shida kwa kuwa inafedhehesha hadi kwa watu ambao unawaheshimu.

"Sina hamu na mikopo ya mitandao, wametuma ujumbe hadi kwa wakwe zangu, ninaonekana mdaiwa sugu na sijui namba za hao watu wametoa wapi wakati sijawapa namba," analalama Zuhura.

Subira Malenda, mkazi wa Mtongani, Dar es Salaam anasema alipopigiwa simu ya kulipa deni, aliwaambia kuwa atalipa ingawa amepitiliza siku moja. Mrejesho kutoka kwao ukawa "tutakukomesha". Wakatuma ujumbe kwa ndugu na jamaa zake kwamba ni mdaiwa sugu.

Latifa Mohamed anasema, "Nilichukua mkopo, nikalipa mara nne, kiwango kikapanda hadi Sh. 260,000, kipanda hadi Sh. 320,000 na ya nne ikafika 376,000.

"Yaani ukichelewa hata siku moja tu, wanakupigia simu unawaambia 'nitalipa baada ya siku mbili na riba', wanakutukana. 'Ulipokuja kwetu ulikuwa mwembamba sasa umenenepa, unaleta dharau'. Unapigiwa simu na zaidi ya watu 40, unatukanwa matusi makubwa makubwa.

"Wanaingilia hadi mawasiliano yako, wanatuma ujumbe kuwa 'huyu ni tapeli, amekopa kwenye kampuni yetu, tunaomba ulipe, maana wewe ni mdhamini wake, tunaliambia Jeshi la Polisi limkamate'.

"Ndugu wanachanganyikiwa, wanafamilia, wakwe, mimi baba yangu alinipigia, akiniambia 'umeshaanza kuwa tapeli?'" anasema.

Latifa anasema aliamua kufunga akaunti yake ya Google, akatupa laini ya simu aliyotumia kukopa, hawakumpata tena kwa simu.

"Kabla ya hapo, waliunda kundi la WhatsApp, wakaweka kitambulisho changu cha NIDA, picha yangu, wakaungisha namba za simu zilizokuwa kwenye 'phone book' yangu kisha wakatangaza kuwa 'huyu ni tapeli'.

"Riba yao ni kubwa, umekopa Sh. 200,000 unalipa hadi Sh. 320,000. Kuna shida nyingine, Kwa mfano, kampuni ya Pesa X nilikopa Sh. 250,000, wakanipa 80,000 ya ziada na baada ya siku tatu wakanipigia 'ukirudisha unapata mara mbili ndani ya saa 24, nikalipa wakanipa mara mbili, baada ya kuchelewa siku mbili, niliwaomba wanipe muda zaidi, ndipo matusi yalianza," anasimulia.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Maji Matitu C, Mbagala, Dar es Salaam, Rashidi Matimbwa anasema aliwahi kushughulisha migogoro miwili ya watu waliokopa mtandaoni, akiwa na ushuhuda wa baadhi ya wananchi walioamua kuhama eneo hilo kutokana na kero ya madeni na udhalilishaji.

"Shida iliyopo ni kwamba wengi wanaona ni rahisi kukopa mtandaoni, lakini kudaiwa wanaona kero. Hii imechangiwa pia na namna wao wanavyodai madeni yao, kwa sababu hata jinsi wanavyodai inakuwa shida," anasema.

Mjumbe mwingine wa Kata ya Kibonde Mbagala, Veronica Mbunde anasema si mgeni wa kinachowasibu wanaokopa mtandaoni, akiwa na ushuhuda wa jirani yake aliyekumbana na vitisho vya wakopeshaji baada ya kukopa na kushindwa kurejesha kwa wakati.

Anasema wakopaji wengi wa mtandaoni hawana elimu ya kutosha kufahamu madhara ya mikopo na nini wafanyie fedha hizo, akisisitiza jambo hilo ni hatari kwa wakopaji.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

## 604 wapimwa, 83 wabainika kuwa na maradhi ya moyo

**Na Christina Mwakangale**

WAGONJWA 83, wakiwamo watoto 21, kati ya watu 604 waliofanyiwa uchunguzi wa moyo mkoani Arusha, wamekutwa na matatizo ya moyo na kupatiwa rufani.

Wagonjwa hao wapewa rufani kwenda kutibiwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) baada ya kubainika kuwa na matatizo hayo wakati wa kambi ya siku tano iliyofanywa kwa kushirikiana na Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC).

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema asilimia kubwa ya watu waliowaona walikuwa na tatizo la shinikizo la juu la damu, yaani presha.

Dk. Kisenge ambaye ni bingwa wa magonjwa ya moyo, alisema wako ambao waliwakuta na shida ya mfumo wa umeme wa moyo, misuli ya moyo kushindwa kufanya kazi, huku watoto wakiwa na matatizo ya valvu na matundu.

"Katika kambi hii, watu wote 604 tuliowaona tuliwafanyia vipimo vya kuangalia jinsi moyo unavyofanya kazi, mfumo wa umeme wa moyo na vipimo vya maabara.

Mkurugenzi wa Magonjwa ya Moyo kutoka taasisi hiyo, Dk. Tatizo Waane alisema miundombinu iliyoko ALMC, iko vizuri na yote inalenga kuboresha afya ya Watanzania na wananchi wa Arusha.

Dk. Waane ambaye ni bingwa wa magonjwa ya moyo, alisema kliniki ya matibabu ya moyo itakuwapo kila siku ALMC na wananchi watapimwa vipimo vyote vya moyo pamoja na kupewa dawa na watakaogundulika kuwa na shida, watapewa rufani ya kwenda kutibiwa JKCI.

Mkurugenzi Mtendaji ALMC, Dk. Godwill Kivuyo alishukuru serikali kwa kuwatuma wataalamu kutoka JKCI kufanya kambi ya upimaji na matibabu ya moyo kwa wananchi wa mkoani humo.

"Kambi hii ya matibabu imefanyika kwa muda wa siku tano na mwitikio umekuwa mkubwa, watu wengi wana shida, wanahitaji kupata huduma za matibabu ya moyo.

# Taharuki yazuka wanafunzi wakianguka ovyo darasani

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

TAHARUKI imezuka katika kijiji cha Ghalunyangu, Kata ya Makuro, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, baada ya mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ghalunyangu kudaiwa anarusha dawa za kienyeji kwenye madarasa na kusababisha wanafunzi wenzake kuanguka ovyo madarasani na kuzirai.

Wananchi walikusanyika na kuazimia serikali ifunge shule hiyo haraka ili kunusuru wanafunzi ambao wanaanguka na kuhatarisha maisha yao.

Diwani wa Makuro, Jumanne Salum, akizungumza na mwandishi wa gazeti hili jana kwa njia ya simu, alisema wanafunzi kuanguka ovyo wanapokuwa shuleni huko kulianza kujitokeza mwanzoni mwa wiki iliyopita.

Alisema kuwa kutokana na mfululizo wa matukio ya wanafunzi kuanguka ovyo, ilibainika kuwa kuna mwanafunzi alikuwa anatembea na dawa za kienyeji na alikuwa akiwaeleza wenzake kwamba akiwapaka, watageuka kuwa nguruwe au mbuzi.

Salum alisema mwanafunzi huyo alipoulizwa kuhusu dawa hizo anazotembea nazo, alidai alipewa na mama yake ambaye naye alizipata kwa mganga wa kienyeji aitwaye Kamba Kasubi ambaye mwezi Septemba mwaka huu alikamatwa na Jeshi la Polisi.

Mganga huyo alikamatwa akituhumiwa kuua watu 10 na kuwazika kwenye makazi yake katika kijiji cha Makuro, wilayani Singida na katika kijiji cha Porobanguma, wilayani Nchemba, mkoani Dodoma kwa nyakati tofauti.

Diwani huyo alisema kutokana na tukio la wanafunzi wa shule hiyo kuanguka ovyo na kumbukumbu ya tukio la mauaji yanayodaiwa kufanywa na mganga huyo, kulizuka taharuki kubwa kwa wananchi wa kijiji cha Ghalunyangu.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, Jumamosi iliyopita alifika katika kijiji cha Ghalunyangu kwa lengo la kuzungumza na wakazi wa kijiji hicho na kufanikiwa kutuliza hasira za wanakijiji.

Mama wa mwanafunzi alikamatwa na Jeshi la Polisi na kuchukuliwa kwa ajili ya mahojiano.

Gondwe, akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, ambao walikuwa takribani 300, alisema serikali haiwezi kukubali kuona shule hiyo inafungwa kutokana na "ujinga unaofanywa na mtu mmoja".

"Anataka tufunge shule ili afurahie. Sasa sisi hatufungi, maana tukifunga atakuwa amefanikiwa ajenda yake, tusikubali ajenda yake ifanikiwe kwani yeye siyo Mungu," alionya.

Katika kuhakikisha suala hilo linakomeshwa, Mkuu wa Wilaya jana alishiriki ibada na sala iliyofanyika shuleni huko ikiongozwa na viongozi wa dini zote na kuwashirikisha wanakijiji wote.

Gondwe aliwaomba wananchi kuendelea kufanya ibada na maombi katika shule hiyo ili kukemea vitendo hivyo vya kishirikina ambavyo vinaweza kuzorotesha maendeleo ya elimu katika shule hiyo.

"Yaani hataki watoto wetu wasisome elimu ambayo sasa ni bure, haina malipo kwa sababu zake, yeye ni Mungu?" alihoji.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

UHURU NA UMOJA

RUFIJI DISTRICT COUNCIL
HALMASHAURI YA WILAYA RUFIJI

Tarehe: 22/10/2024

TANGAZO LA KUSUDIO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji Ndg. Simon Berege anawatangazla wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kuwa, Serikali inakusudia kupandisha hadhi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kuwa Halmashauri ya Mji Rufiji

Notisi ya kusudio imetolewa katika Gazeti la Serikali Namba 818 la mwaka 2024 la tarehe 20 Septemba 2024 Mwananchi mwenye pingamizi juu ya kusudio hili afikishe pingamizi lake kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ndani ya siku 60

EXECUTIVE DIRECTOR
RUFIJI DISTRICT COUNCIL

Simon Berege

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wananchi sasa ni wakati wa kuhakiki majina waliojiandikisha

**UANDIKISHAJI** wa Daftari la Wapigakura la Wakaazi, umekamilika mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kujiandaa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Umuhimu wa kujiandikisha kwenye daftari hilo ni kutoa haki kwa wananchi wote wanaostahili kupiga kura kuchagua viongozi wao wa mtaa wanao ona wanaweza kutatua kero zao. Uchaguzi huu ni muhimu kwa kuwa kero zote za mitaa zinapaswa kushughulikiwa kuanzia ngazi za mitaa kwa sababu viongozi watakaochaguliwa ndio wako karibu na wananchi na ni rahisi kuwafikia kwenye mitaa yao.

Kupitia uandikishaji uliofanyika, jukumu la kila kituo ni kubandika majina yote ya watu waliojiandikisha na kisha wananchi wanapaswa kuyahakiki ili kuona yako sahihi na kama kuna watu ambao wamejiandikisha, lakini hawastahili kwa kukosa sifa, itolewe taarifa ili ifanyiwe kazi kuondoa malalamiko.

Moja ya kigezo cha kukosa sifa ya kujiandikisha kwenye daftari hilo ni kama aliyejiandikisha, hajafikisha umri wa miaka 18 na sio raia wa Tanzania na mkazi wa mtaa husika.

Watu wengi wamekuwa wakijiuliza mbona wakati wa kujiandikisha mtu alikuwa akiulizwa majina yake na mtaa anaoishi tu bila uthibitisho mwingine. Ufafanuzi uliotolewa ni watu kwenda kwenye vituo na kuhakiki majina yao na wale wanaoonekana kama hawastahili wawekewe pingamizi kwa uthibitisho. Imeelezwa kuwa kwenye uandikishaji ilihakikishwa kuwa kuna mawakala wa vyama ambao walipewa fursa ya kuhakikisha wanaojiandikisha ni wakazi halali wa mitaa hiyo.

Hivyo, imefafanuliwa kuwa wasiwasi kwamba kunaweza kukatokea udanganyifu wa watu wasiokuwa na sifa ya kujiandikisha wanaweza kujipenyeza uondolewe. Kwa muda huu ambao majina yatabandikwa vituoni ni vyema wananchi wakatumia fursa hiyo kujitokeza kwenda kuhakiki majina ili kuondoa usumbufu wakati wa kupiga kura unapowadia. Ni jukumu pia la wahusika kwenye mitaa na viongozi kutoa ushirikiano katika hili ili kuondoa malalamiko na sintofahamu wakati wa uchanguzi.

Uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu sana kwa wananchi kwa sababu kero nyingi huanza kutatuliwa kwenye mitaa na zinaposhindika ndio huenda kwenye ngazi za juu.

Viongozi wanaochaguliwa ni lazima watimize wajibu wao kwa kushirikiana na wananchi wanaowachagua na kusikiliza kero kwa kuzitatua au kutoa taarifa kwa wananchi wao pale kunapojitokeza changamoto ya aina yoyote ile.

Mara nyingi wananchi wamezoea kuona viongozi wanapochaguliwa wanabweteka kwa kutotoa ushirikiano hata wanapofikishiwa kero mbalimbali zikiwamo za miundombinu mibovu ya barabara kwenye mitaa, tatizo la ulinzi na usalama hali inayosababisha wananchi hao kupoteza imani kwao. Viongozi wengine wanapoona wananchi wanachukua uamuzi wa kutatua kero hizo kwa kuamua kujichangisha na kutengeneza barabara au kuweka ulinzi, wanadhani kuwa wanataka kunyang'anywa nyadhifa zao.

Wengine hata kuitisha mikutano na wananchi wao ili kujua kero zao wanashindwa na badala yake wanasubiri unapokaribia uchaguzi ndio wanaitisha kikao tena ni cha kutoa lawama badala ya kujibu kero wanazopelekewa.

Wananchi wanapokwambia kiongozi kwamba kwenye mtaa wetu kuna kikundi cha vijana wanaofanya uhalifu, fuatilia na chukua hatua tena kwa kuwashirikisha wananchi wako. Ukifanya hivyo hata kazi yako itakuwa rahisi na wananchi watakupenda kwa sababu umeonesha kuwajali, kuwasikiliza na kutatua kero zao. Miundombinu ya barabara inapoharibika, kiongozi unapaswa kuwashirikisha wananchi wako ili uweze kusaidiwa na kufanya kazi yao iwe rahisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

## Wajasiriamali sokoni hebu kuweni wasafi

**USAFI** ni jambo jema kwa vile kwenye taka kuna wadudu kuanzia wanaotambaa hadi wanaoruka lakini pia kuna harufu.

Lakini inashangaza mfanyabiashara yuko pembeni anauza bila kujali kuwa anapouzia ni pachafu na ni kero kwake na wale anaowahudumia.

Katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu, ndiko kuliko na fursa. Utakubaliana nami unaposhuhudia idadi kubwa ya watu hususan maeneo yenye shughuli muhimu. Ni kwenye masoko, vituo vya daladala na mabasi ya masafa, viwanja vya michezo na karibu na shule.

Maeneo haya wajasiriamali wengi huyatumia kama vyanzo vya mauzo kwa kuwa katika idadi hii kila mmoja atakuwa na mahitaji yake.

Wafanyabiashara hawa ambao wengi wao wapo katika kundi la wajasiriamali wadogo, utakutana na wauza vyakula, vinywaji, bidhaa za majumbani, vifaa vya kielektroniki, nguo, viatu na mahitaji ya shuleni. Pamoja na serikali kutoa vibali na baadhi ya wajasiriamali hawa kupatiwa vitambulisho kufanya biashara maeneo haya, kuna changamoto ya usafi na utunzaji wa mazingira yanayozunguka maeneo haya.

Ukifika vituo vya daladala, mfano Kariakoo, Makumbusho, Gongo la Mboto vyote vya Dar es Salaam utashuhudia tatizo hilo kwani wengi kwenye biashara zao hawajali usafi cha muhimu pesa kwanza. Pia maeneo ya soko Tandika, Kariakoo, Manzese, Urafiki, Tandale na Buguruni Dar es Salaam, unakutana na uchafu usiopendeza machoni.

Jamani kumbukeni mtu ni afya, kuzitunza afya za wateja na unayeuza bidhaa ni kitu muhimu. Wachuuza wanapoanza biashara asubuhi, hawafanyi usafi utadhani ufagio ni adui.

Wamekaa pembeni ya rundo la taka za matikititi, machungwa, maganda ya mahindi, ndizi, vifungashio, maboksi na majini mabichi yanayofungia bidhaa.

Ingekuwa ni bora fursa iendane na wajibu, sababu fursa wamepewa wajasiriamali hawa ambao kundi kubwa ni vijana, siku hizi mjini wanasema 'kujiongeza'.

> **Mbona katika vyoo vya kulipia utalipia gharama ya Sh. 300 hadi 500 lakini baada ya kutumia choo iwe haja ndogo au kubwa, utaacha umemwagia maji au kusafi.**

Wafanyabiashara mjiongeze katika maeneo yenu ya biashara kwa kila mmoja kuwa na chombo cha kuhifadhi taka yaani vikapu, ndoo au beseni kutunza taka zenu, si sawa hata kidogo uzalishe uchafu tena kila dakika usubiri waje wakufagilie.

Kuna ambao watasema tunalipa ushuru. Ni sawa ushuru unalipwa, lakini akija mfanya usafi akute pa kuanzia, labda taka zimetunzwa mahali fulani atazikusanya na kumalizia kufagia. Ni sawa na kusema ukilipia ushuru, uache eneo chafu au mazingira machafu. Mbona katika vyoo vya kulipia utalipia gharama ya Sh. 300 hadi 500 lakini baada ya kutumia choo iwe haja ndogo au kubwa, utaacha umemwagia maji au kusafi.

Ni wachache wasio na uelewa wakaacha choo kichafu na kumfanya anayeingia baada yako arudi nyuma kama ameona chatu chooni.

Jamani hata wanaokuja kufanya usafi katika maeneo yenu ya biashara iwe soko au vituo vya daladala ni watu kama wengine, ambao wanahitaji kukuta utaratibu uliowekwa na wewe mzalisha uchafu kisha zikabebwa na gari taka hadi Pugu dampo.

Kituo kipya cha Mwenge, Dar es Salaam, ni kizuri na usafi pia upo, kitakaposhamiri kwa kutoa huduma je, usafi utaimarika?.

Wajasiriamali, wafanyabiashara kuweni rafiki wa mazingira kwa kuwa wasafi na muwe na vyombo vya kuhifadhia taka ngumu, na si kutupa taka barabarani. Hii inawachanganya hata wafagizi wa barabara ambao yeye huja na toroli, mfagio na koleo ili aweze kuzoa mchanga akishafagia, huchanganyikiwa anakutana na maganda ya miwa, ndizi au makopo akijiuliza azoe mchanga au taka ngumu.

Wafanyabiashara hiyo ndio ajira ambayo isiyo rasmi lakini inatambulika kwa kuziwezesha familia zenu kupata mahitaji na ni maendeleo pia kwa nchi, lakini kumbukeni mtu ni afya na maofisa afya wachukue hatua.

# Bil. 14/- zatengwa kupata wataalamu matibabu kibingwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI kupitia Mpango wa Ufadhili wa Masomo ujulikanao Samia Health Specialization Scholarship Program, imetenga Sh. bilioni 14 ili kufanikisha azma ya kuwa na wataalamu wa kutosha wa matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ndani ya nchi.

Jitihada hizo zimelenga kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, kupunguza rufani za matibabu nje ya nchi na kupunguza gharama kwa serikali na wananchi pamoja na kuvutia tiba utalii.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mpango huo wa serikali kusomesha wataalamu bingwa na wabobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha.

"Katika kufanikisha azma ya kuwa na wataalamu wenye ujuzi wa kutosha wa kutoa huduma bora za matibabu hapa nchini, Wizara ya Afya ilijiwekea lengo la miaka mitano (2020-2025) la kusomesha wataalamu bingwa na wabobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha. Kupitia Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Serikali unaojulikana kama Samia Health Specialization Scholarship Program," alisema Mhagama.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2024/2025, serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga jumla ya Sh. bilioni 14, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 3.05 sawa na asilimia 28 zaidi ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ya Sh. bilioni 10.95.

"Fedha hizi zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zitatumika kugharamia mafunzo kwa wataalamu wapya 544 kwa mafunzo ya Ubingwa na Ubingwa bobezi pamoja na wataalamu wengine 47 kwa utaratibu wa seti," alisema.

Kadhalika, alisema wataalamu 829 wanaoendelea na masomo ya ubingwa na ubobezi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi wataendelea kupewa ufadhili kupitia fedha hizo.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha wizara ilipokea jumla ya maombi ya ufadhili 948 nchi nzima, kati ya hao waombaji wa jinsia ya kike ni 353 sawa na asilimia 37 na ya kiume ni 595 sawa na asilimia 63.

"Kati ya hao, waombaji 771 walikidhi vigezo vya kufadhiliwa na waliochaguliwa kwa ajili ya ufadhili ni 544 sawa na asilimia 71 ya waombaji waliokidhi vigezo," alisema.

Mhagama, alisema kati ya watumishi 544 waliochaguliwa kupata ufadhili, jinsi ya kiume ni 338 sawa na asilimia 62 na ya kike ni 206 sawa na asilimia 38.

Alisema, watumishi waliochaguliwa kupata ufadhili katika vyuo vya ndani ya nchi ni 517 sawa na asilimia 95 na nje ya nchi 27 sawa na asilimia tano.

"Kwa takwimu hizi, kumekuwa na ongezeko la kufadhili watumishi wanaoomba kusomeshwa na serikali kutoka asilimia 56 mwaka 2022/2023 hadi 71 mwaka 2024/2025.

"Serikali ya awamu ya sita kwa kuona umuhimu wa uwekezaji katika sekta ya afya imeshatumia jumla ya shilingi bilioni 30.95 katika kuendeleza wataalamu bingwa na bobezi katika sekta ya afya nchini," alisema.

Alisema, wizara imezingatia vipaumbele muhimu vya kisekta katika ubobezi katika ngazi mbalimbali za huduma pamoja vipaumbele kama vilivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa tano wa Sekta ya Afya pamoja na bajeti ya wizara ya mwaka 2024/25.

Alisema vipaumbele hivyo ni pamoja na taaluma za watoto wachanga, afya ya akili, magonjwa yasiyoambukiza kama magonjwa ya moyo, matibabu ya ubongo na mishipa ya fahamu, huduma za utengamao na tiba shufaa.

## Wadau usafirishaji, utalii watakiwa kutunza mazingira

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa usafirishaji na utalii nchini wamekumbushwa kuhakikisha kuwa maendeleo ya sekta hizo hayasababishi uharibifu wa mazingira nchini.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Usafirishaji na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama cha Mawakala wa Usafiri Tanzania (TASOTA), jijini Dar es Salaam.

Tukio hilo la siku mbili linawaweka pamoja wadau wakuu kutoka sekta za usafiri na utalii kwa ajili ya majadiliano ya kina na kubadilishana mawazo namna ya kuendeleza sekta ya utalii nchini.

Kihenzile alisema usafiri na utalii ni miongoni mwa sekta muhimu nchini na zina wajibu wa kuhakikisha ukuaji wake ni endelevu usioathiri mazingira.

"Ukuaji wa sekta ya usafiri na utalii lazima uendane na uendelevu. Ni wakati ambapo masuala ya mazingira si ya pili tena, lakini yanachukuliwa kama sehemu ya msingi ya mikakati ya biashara," alisema.

Aidha, aliwaelekeza wadau wa sekta hiyo kuonesha mfano kwa kuwekeza kwenye utalii endelevu na unaowajibika kama vile kujenga mazoea endelevu ya kuanzisha mipango ya kupunguza utoaji wa hewa.

"Uwezo wa utalii wa Tanzania ni mkubwa, na tuna kila fursa ya kujiweka katika jukwaa la kimataifa kwa kukumbatia mada hii ya uvumbuzi, ukuaji na uendelevu," alisema.

Alisema ni matumaini yake kwamba, mijadala katika kongamano hilo itaweka msingi wa mikakati ambayo pia itahakikisha ukuaji huo unakuwa jumuishi endelevu na kibunifu.


## TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR

87 Barabara ya Binguni
Binguni S.L.P 1439
Postcode: 72214, Binguni
Zanzibar

Tel: +255 (0) 776 264 880
Barua pepe: info@zahri.go.tz
Tovuti: www.zahri.go.tz

## TANGAZO LA KAZI

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) imeanzishwa kwa Sheria namba **5** ya mwaka **2020.** Taasisi hii ni miongoni mwa Taasisi muhimu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Taasisi ya Utafiti wa Afya ina jukumu la kufanya tafiti na kusimamia upatikanaji wa taarifa za kisayansi kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha njia mbalimbali za tiba na udhibiti wa magonjwa ya binadamu nchini.

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) inatangaza nafasi ya kazi kwa mkataba wa miaka mitatu (3) kama ifuatavyo: -

Mtafiti Mkuu (Senior Resercher) nafasi moja (1)

**Sifa za Muombaji**

i. Awe raia wa Tanzania au nchi yoyote nje ya Tanzania.
ii. Awe mwenye kiwango cha elimu ngazi ya Uzamivu (PhD).
iii. Awe amefanya kazi katika taasisi za Tafiti na mwenye uzoefu wa kazi za tafiti usiopungua miaka kumi (10)
iv. Awe ameandika miradi ya tafiti na kushinda angalau miradi mitatu (3)
v. Awe amechapisha angalau machapisho matano (5) katika jarida la Sayansi linalotambulikana **"Scientific Conference Proceedings".**

**Majukumu:**

i. Kufanya Utafiti wa Afya uliothibitishwa kwa mujibu wa fani husika kwa kukusanya taarifa, kuchambua na kuandika ripoti;
ii. Kuandaa mapendekezo ya Tafiti bora za Afya (Research Proposals) zitakazowavutia wafadhili;
iii. Kuhakikisha uwasilishwaji wa mapendekezo ya Tafiti katika "Institutional Review Board" (IRB) kwa ajili ya kuthibitishwa;
iv. Kutoa mafunzo kwa Watafiti wasaidizi katika kuandaa mapendekezo ya Utafiti;
v. Kusambaza matokeo ya Tafiti katika maeneo tofauti ikiwemo kuchapisha kwenye majarida ya kisayansi pamoja na mikutano ya Kisayansi;
vi. Kushiriki katika Mikutano ya Kisayansi kwa ajili ya kubadilishana taarifa za Kitafiti;
vii. Kupanga, kutekeleza na kuendeleza kazi za Utafiti kwa mujibu wa miongozo ya Taasisi;
viii. Kuboni njia bora za Tafiti kibiashara kwa ajili ya kuimarisha afya ya binaadamu;
ix. Kutafuta fursa kwa ajili ya ushauri elekezi kwa lengo la kutekeleza mikataba ya Kitafiti iliyozawadiwa;
x. Kushiriki katika kutengeneza na kutoka mafunzo katika fani husika;
xi. Kushiriki katika kupitia na kutengeneza mpango mkakati, Bajeti na vipaombele vya Tafiti za Afya;
xii. Kushiriki katika maswala ya Tafiti za Afya baina ya Taasisi za Umma na Binafsi kwa lengo la kuimarisha na kukuza Afya ya Binadamu;
xiii. Kufanya kazi nyenginezinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**Vigezo na masharti kwa muombaji.**

1. Muombaji awe Mtanzania au kutoka nje ya Tanzania.
2. Muombaji aambatanishe vivuli vya maelezo binafsi yanayojitosheleza ( Detail CV), vyeti vya kumalizia masomo, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Mkaazi (ID) au nakala ya hati ya kusafiria (Pasport).
3. Atakaewasilisha Statement of Result au Progressive Report maombi yake hayatazingatiwa. Maombi yatumwe kwa mfumo wa barua pepe: info@zahri.go.tz na yaelekezwe kwa Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Afya, Binguni Zanzibar.
4. Muda wa mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 31/10/2024 ndani ya muda wa kazi.
5. Taarifa zaidi zinapatikana katika website ya www.zahri.go.tz

**Angalizo.**

Waombaji wote mnasisitizwa kuwa makini mnapowasilisha maombi yenu kwa kuhakikisha masharti na vigezo yanazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuambatanishwa nyaraka zote zinazohitajika.

**Limetolewa na:**
**Bernad P. Mtuta.**
**Mkurugenzi Rasilimali Watu na Utawala,**
**Taasisi ya Utafiti wa Afya**
**Binguni - Zanzibar**
**21 October, 2024.**

# Radi yaua mama, aacha kichanga

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kitongoji cha Sang'ang'a Kijiji cha Nyabisaga, Kata ya Pemba, Tarime mkoani Mara, Koreda Maryoba (34), amefariki dunia baada ya kupigwa na radi akiwa ndani ya nyumba.

Akisimulia tukio hilo mume wa marehemu, Saiya Maryoba, alisema alifikwa na umauti siku ya Ijumaa jioni wakati mvua ikiendelea kunyesha baada ya kupigwa na radi na kufariki papo hapo.

"Nimepata pigo kubwa kwa kumpoteza mke wangu, ameniachia hawa watoto wadogo wanne na kichanga ninamwomba Mwenyezi Mungu anitie nguvu niwalee vyema watoto aliowaacha nawashukuru wananchi mliofika hapa kunihani Mungu awe nanyi," alisema Maryoba kwa masikitiko huku akitokwa machozi.

Akizungumza wakati wa maziko, Diwani wa kata hiyo, Seronga Wangwe, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari wakati wa mvua ambayo imeanza kunyesha wilayani hapo ili kuepuka majanga kama hayo.

"Kifo cha mama huyu kimeacha pigo kubwa kwa familia na jamii yetu ya hapa kijijini kwani alikuwa ni nguvu kazi katika kuchangia kuleta maendeleo ninawaasa na kuwahimiza wananchi kuchukua tahadhari wakati wa mvua inaponyesha," alisema.

Alitaja namna ya kukabiliana na hali hiyo kuwa ni pamoja na kuepuka kukaa chini ya miti wakati wa mvua, kutoongea na simu, watoto kutocheza nje wakati mvua ikiendelea kunyesha na kukaa mahala salama ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza wakati mvua.




Meneja Uhusiano wa Airtel, Jackson Mbando (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuzindua msimu wa tano wa mashindano ya mamalishe, yatakayoanza Oktoba 30, mwaka huu katika viwanja vya Mwijuma Mwananyamala. Kulia ni Mkuu wa Lipa kwa Simu Airtel Money, Victory Makere na Mtangazaji wa East Africa TV na Radio, Yusta Msowoya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwekezaji kulima miti ya mianzi Pwani

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, amesema miti ya mianzi itaanza kulimwa kwa wingi nchini na wawekezaji kutoka nchini Uswisi.

Aidha, amesema lengo ni kulikamata soko la dunia, kwa kuwa ni mali ghafi imara na nafuu kwenye matumizi ya ujenzi wa majengo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa mradi wa upangaji wa miti hiyo unaotarajiwa kuanzia Kibaha, mkoani Pwani utakaogharimu Sh. bilioni 280.

Alisema serikali inaunga mkono juhudi za uwekezaji huo, kwa kuwa una manufaa kwa wananchi na nchi kwa ujumla, na kuwa mmoja wapo ya kuboresha ujenzi wa nyumba kwa gharama nafuu.

"Serikali inaendelea kuwathamini wawekezaji wote ndiyo maana uwekezaji unakwenda vizuri unavutia wawekezaji kutokana na sera nzuri, wawekezaji wote ni muhimu, wa ndani ni wazawa ndiyo wenye nchi, wageni wanatuletea fedha za kigeni," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Shikana Group, Amne Kageshi, ambayo ni washauri wa wawekezaji wa mradi huo, Silver Terra, alisema katika awamu ya kwanza ya mradi wamekusudia kuwekeza kwenye kilimo hicho Dola za Marekani milioni 50 na vijana takribani 5,000 watapata ajira za mikataba.

"Tunatarajia kuwekeza kilimo hiki kwenye hekta 25,000 ni eneo kubwa, tutaanzia na hekta 8500 Kibaha, mianzi ni mmea ambao unaweza kuotesha sehemu yoyote haihitaji mambo mengi bali maji tu," alisema Kageshi.



Kwa sasa unafanyika upembuzi yakinifu, mwakani ndiyo wataanza kupanda mimea hiyo, zao hili kuwa la biashara ni kitu kipya, lakini linajulikana kwenye soko la dunia, inatumika hadi kwenye ndege na baadhi ya maeneo.

Mkurugenzi wa Silver Terra Carl-Lambert Liesenberg alisema nia yao ni kuungaisha shughuli za kiuandisi ujenzi wa Uswizi na Tanzania, ikimaanisha kwamba wanaweza kuendeleza ujenzi wa majengo kwa miti ya mianzi kwa ujuzi wao wa Uswizi.

Aidha, alisema ni malighafi nafuu inayoweza kutumika kwenye ujenzi wa kisasa, pia ni rafiki wa mazingira hasa katika kipindi hiki ambacho ulimwengu unaangaika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, tumefanya utafiti na tumejiridhisha kuwa malighafi ina gharama nafuu lakini ni imara pia.

Meya wa Manispaa ya Kibaha, Mussa Ndomba, alisema mradi huo ni neema hasa kwa vijana kwa kuwa itatoa fursa ya kupata ajira, na kujifunza kilimo hicho hivyo nao wanaweza kulima kwenye maeneo hayo hasa wakiwa na uhakika na soko, lakini utasaidia kutunza mazingira.

"Kibaha ni eneo la kiuwekezaji kimsingi nafikiri linaongoza iwe katika kilimo au viwanda Tanzania yote ni eneo la kimkakati, kila unachokusudia kukifanya kuhusu uwekezaji kinawezekana, kwa hiyo tunaendelea kukaribisha wawekezaji," alisema Meya Ndomba.

## Mchechu achangisha mil. 117.8/- ujenzi wa kanisa

**Na Mwadishi Wetu**

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, ameendesha harambee iliyowezesha kuchangisha Sh. milioni 117.8 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Naibili, Siha, Kilimanjaro.

Kati ya fedha hizo Sh. milioni 50.2 ni taslimu, Sh. milioni 66.5 ni ahadi na Sh. milioni 1.1 zilipatikana kwa njia ya mnada.

Mchechu ambaye anayejulikana kwa mchango wake mkubwa katika sekta ya nyumba, benki na biashara, katika harambe hiyo iliyofanyika Jumapili iliyopita, pia ilipatikana mifuko 118 ya saruji.

Fedha na saruji ni kwa ajili ya upanuzi wa jengo hilo la ibada na kazi ya plasta, kwa mujibu wa Askofu Dk. Fredrick Shoo, Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT. Kazi hizo mbili za upauzi na plasta, zinatarajiwa kugharimu Sh. milioni 150.

Akizungumza na viongozi wa dini, serikali, kijamii na waumini wa Naibili, Mchechu alisema haja ya kuendelea kuwa na moyo wa kutoa na kushirikiana mpaka ujenzi wa nyumba hiyo ya ibada utakapokamilika.

"Tunapoendelea na ujenzi huu, nataka niwaombe ninyi wapendwa msiishie hapa. Tuendelee kufanya kazi kwa pamoja mpaka ujenzi utakapokamilika," alisema.

"Kanisa bado linahitaji michango yenu, maombi yenu, na utayari wenu wa kujitoa. Kila mmoja wetu anaweza kutoa kitu, iwe ni fedha, muda, au huduma kwa namna yoyote ile."

Alisema ikiwa watatoa kwa moyo wa upendo, Mungu atarudisha zaidi na vikombe vyao vitafurika.

Alisisitiza kwa kunukuu Biblia katika Luka 6:38: "Wapeni watu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa, cha kusukwasukwa, na kushindiliwa, na kufurika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu."



# Ukatili kiuchumi mwiba zaidi kwa wanawake

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UKATILI wa kiuchumi, unatajwa kuwa mwiba zaidi kwa wanawake wanaotoka Kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro kumiliki.

Aidha, suala la jinsia, hasa haki ya kuchagua na kuchaguliwa, likiendelea kuathiriwa na mfumo dume.

Kutokana na hali ilivyo, vikundi mbalimbali vya wanawake wa Kijiji cha Lole, wamegeuka waelimishaji kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, ili kusukuma ajenda ya wanawake kuingia katika nafasi za maamuzi kushughulikia changamoto za ukatili wa kingono na kiuchumi.

Changamoto hiyo ya kuendelea kushamiri kwa ukatili huo, iliibuliwa jana na wanawake wa Lole, wakati wa kikao kazi cha wadau wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la kiraia la KWIECO, linalofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT).

Akizungumzia ukatili huo, Loveness Shao alisema bado wanaume wa Marangu, hawaamini kama mwanamke anaweza kurithi mali, hivyo wanatamani kuutumia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu 2025 kupata wanawake watakaokuwa na sauti katika meza ya maamuzi.

Mary Mremi alisema ili kukabiliana na ukatili wa kiuchumi na kingono dhidi ya wanawake na watoto, ni vizuri kupata wanawake jasiri na imara katika uchaguzi wa serikali za mitaa watakaozuia na kubadili fikra, mitazamo na tabia.

Wakati, Lilian Mringo alisisitiza wanawake wakijumuishwa katika nafasi za uongozi, watakuwa chachu ya kushughulikia ufumbuzi wa tatizo linapotokea, pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji haki na mbinu zinazozingatia kuponya majeraha ya waathirika wa ukatili.

Katika kikao kazi hicho, Ofisa Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa wa KWIECO, Peter Mashingia, alisema ukatili dhidi ya wanawake upo, na ukatili dhidi ya vijana wa kike upo, kwa kuwa takwimu zinaeleza katika hatua tatu, wanawake watatu au vijana watatu wa kike, mmoja wao lazima amefanyiwa ukatili.

"Na katika huyo mmoja aliyefanyiwa ukatili, unaweza kukuta ni mara chache sana katika kundi la wanawake 10 wakapeleka taarifa hiyo katika vyombo husika. Kwa mfano katika wanawake 10 waliofanyiwa ukatili wa aina yeyote ile unakuta labda ni wawili tu au watatu watatoa taarifa.Tafsiri yake ni kwamba mambo mengi sana yanaishia chini na taarifa nyingi hazitolewi."

Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaolenga kuendeleza majukwaa ya wanawake kwa ajili ya haki za uongozi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, Veronica Ollomi, alisema mradi huo utashughulikia pamoja na mambo mengine ajenda ya kumaliza masuala ya unyanyasaji wa kingono, unyonyaji wa kiuchumi na kukuza wanawake katika nafasi za uongozi.

"Tutaongeza uelewa wa jamii kuhusiana na masuala ya sheria, masuala ya ukatili wa kijinsia na mbinu za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo ambayo tutayafanyia kazi.

"Tunajua katika mchakato kama uchaguzi kuna rushwa ya ngono na rushwa tofauti. Je, yeye kama mwanamke anayetamani kuwa kiongozi akabiliane vipi na hizo changamoto ambazo zinaweza zikajitokeza katika mchakato mzima wa kugombea hizo nafasi za uongozi."

Kwa mujibu wa Veronica, Kata zinazoguswa na mradi huo ni Pasua na Ngangamfumuni (Manispaa ya Moshi), na Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi).

## Wananchi Muheza wafurahia kambi matibabu ya Rais Samia

**Na Steven William,** MUHEZA

KAMBI ya siku sita ya matibabu ya kibingwa, inayotumiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kupunguza gharama za wananchi kusafiri umbali mrefu kwenda hospitali za kanda na kitaifa, kufuata huduma za uchunguzi na tiba, imetua katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga.

Mabingwa hao wanatajwa kuwa mwarobaini dhidi ya rufani za tiba zinazotolewa katika ngazi ya Hospitali za Wilaya ya Mikoa.

Akizungumzia ujio wa madaktari hao maarufu kama 'Madaktari Bingwa wa Mama' Mkuu wa Wilaya hiyo, Zainab Abdallah, jana alisema kuwa watatoa huduma za uchunguzi kwa watoto na watoto wachanga pamoja na huduma za afya ya uzazi, wajawazito na magonjwa ya wanawake.

Alisema uchunguzi huo wa kibingwa, utafanyika kuanzia jana hadi Oktoba 26 mwaka huu, katika eneo la Lusanga, ilipojengwa Hospitali ya Wilaya hiyo.

Mbali na uchunguzi huo, kambi hiyo hujenga uwezo kwa madaktari wenyeji waliopo kwenye vituo kwenye maeneo mbalimbali ya kutoa huduma.

"Kwa sisi wananchi wa Muheza, hii ni fursa adhimu, tunatambua kabisa kuwa huduma mlizoletewa na wataalamu wetu wa afya, zinaonyesha ni kwa kiasi gani Rais Samia, ana mapenzi mema na wananchi wa Muheza," Zainab.

Awali, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo (DMO), Dk. Fani Mussa, alisema mabingwa hao wanatoa huduma ya uchunguzi na tiba kwa magonjwa ya shinikizo la damu na kisukari, huduma za upasuaji, ganzi na usingizi na magonjwa ya kinywa na meno.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian (wa nne kushoto), akikata utepe kwa ajili ya kuzindua magari yatakayotumiwa katika mpango wa huduma za afya zitakazotolewa kwa wiki moja na madaktari bingwa wa Rais Samia kwenye halmashauri 11 za mkoa huo, jana. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Namna ongezeko la tindikali linavyoathiri ardhi ya kilimo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ARDHI mahususi kwa ajili ya shughuli za kilimo katika Mkoa wa Manyara, inatishiwa na ongezeko la tindikali kwenye udongo kwa zaidi ya asilimia 55.

Kemikali hiyo inatishia kufifisha uzalishaji na kuathiri mazao, kuanzia kwenye mizizi.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Utafiti wa Udongo Tanzania kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Sibaway Mwango, eneo la udongo lililoathiriwa ni hekta 300,000 zinazolimwa zao la mpunga, ambako chumvi na magadi vimetanda juu ya udongo.

"Udongo ukiwa na athari ya chumvi chumvi, magadi na tindikali, uzalishaji unakuwa chini sana kwa wakulima na kuwasababishia hasara,"alifafanua Dk. Mwango.

Aidha, alisema kwanini uzalishaji unakuwa chini ni kwasababu kiwango kikubwa cha mbolea kinapotea kwenye udongo.

"Tindikali ikiwa hali ya juu mbolea inapotea mpaka asilimia 70 kwenye udongo na kiwango kinachobakia ni asilimia 30,"alieleza.

Mtafiti huyo alisema wakulima unakuta wanalalamika eti mbolea ni feki kumbe siyo feki ni matumizi ya tindikali kwenye udongo.

Pia alieleza kuwa mimea nayo inaathirika mpaka unakuta mizizi inakuwa kama ina ukoma na inashindwa kuchukua virutubisho kwenye udongo.

Dk. Mwango alisema katika mashamba ambayo yameathirika na tindikali wakulima wanawashauri watumie chokaa kilimo.

"Ili tindikali iweze kushuka na ipungue mbolea iweze kufanya kazi kwa ufanisi mkulima ni vyema kupima afya ya udongo ili ajue," alisema.

Vilevile, alisema kwa mujibu wa utafiti walioufanya mkoani Geita, wameonyesha mkulima anaweza akaweka chokaa kilimo tani moja kwenye hekta 2.5.

Wakati, chokaa ni bei rahisi sana kwa bei ya kiwandani ni Sh. 7,000 mfuko wa kilogramu 50 ila ikikutwa dukani ni Sh. 12,000 kwa mfuko huo hivyo mifuko 20 ambayo inaweza kugharimu Sh. 240,000 inatosha kwa hekta 2.5.

Naye Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika cha mkoani Manyara cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Pendael Valentine, alisema kwa sasa RIVACU inahamasisha wanachama wake kupima afya ya udongo ndio waweze kujua mbolea ya kutumia.

Meneja huyo alisema kilimo ni biashara mkulima asipofuata kanuni za kilimo atapata hasara.





# Milolongo yatajwa kukwamisha upatikanaji mikopo asilimia 10

**Na Remmy Moka,** MWANZA

WANUFAIKA wa mikopo ya asilimia kumi inayotolewa na serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kutoka Kata ya Mkolani, Nyamagana mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuweka wepesi wa upatikanaji wa mikopo hiyo tofauti na milolongo mirefu inayokwamisha baadhi ya wahitaji wanaokuwa na uhitaji katika shughuli za uzalishaji.

Walibainisha hayo juzi wakati wakipatiwa elimu ya matumizi sahihi ya mikopo hiyo inayotolewa na serikali kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili itumike kwa lengo husika.

Mmoja wa wanufaika hao, Marry Robert alisema upatikanaji wa mikopo hiyo unachukua muda mrefu tofauti na mikopo mingine kwani milolongo imekuwa mirefu hadi wanafaika kupata mikopo waliyoomba.

Alisema katika mabadiliko yaliyofanyika ni vyema pia serikali ikaweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa mikopo kwa urahisi, kwani wakopaji wengi wamekuwa wakikata tamaa ya ukopaji kwasababu ya uwepo wa mizunguko mingi hadi mkopaji huyo kupata mkopo aliomba.

Aidha, mnufaika mwingine Mkazi wa Nyanzobe, Nibizi Fabian, alisema licha ya kuchelewa kwa fedha hizo bado kuna baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo hawana elimu ya kutosha ya matumizi sahihi ya ukopaji na utumiaji wa mikopo hiyo jambo linalopelekea mikopo hiyo kutotumika ipasavyo kwani vijana wengi hawapendi kujiunga na vikundi kwa sababu ya ukosefu wa elimu stahiki huku baadhi yao wakituhumu uwepo wa mifumo mibovu ya utolewaji wa mikopo.

Aliongeza kuwa ni vyema serikali isikazie tu katika utoaji mikopo kwenye vikundi pekee ni muhimu pia ikatamaza utoaji mikopo kwa mjasiriamali mmoja mmoja kwani baadhi yao wanao uwezo wa kumudu marejesho ya mikopo hiyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Mkolani, Glory Mbise, alisema baadhi ya wakopaji wamekuwa wakihitaji mikopo, lakini hawafuataji taratibu za ukopaji na matokeo yake wanabaki kulalamikia suala la ukosevu wa mikopo hiyo.

Aidha, aliwataka kufuata taratibu za upatikanaji wa cheti cha mkopo, sheria na kanuni zote zinazohitajika kufuatwa na mkopaji, ili kusaidia kuondoa malalamiko.

Diwani wa Kata ya Mkolani Dioniz, James Swalala, alisema malengo ya serikali ni kuhakikisha inakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla hivyo aliwataka wanufaika wa mikopo hiyo kutumia kwa makusudio lengwa ya serikali kwani itasaidia kukuza uchumi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.



Wakazi wa Kata ya Charambe, Dar es Salaam, wakihakiki majina yao walioandikisha katika Daftari la Mkaazi ambayo yamebandikwa kwenye ukuta wa ofisi ya mtendaji wa kata hiyo, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wosia watajwa chanzo migogoro ya familia, watoto mitaani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TABIA ya wananchi kutokuandika wosia mapema imetajwa kuwa chanzo cha ongezeko la migogoro ya kifamilia pamoja na watoto wa mitaani kutokana na kutokutambuliwa na ndugu wanaopewa usimamizi wa mirathi.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Kutetea Haki za Binadamu (SHIHABI), Onesmo Daudi, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake na kueleza kuwa wanaonyanyasika zaidi ni watoto pamoja na wajane.

Aidha, aliwataka wakazi wa wilayani Kahama, kuhakikisha wanaandika wosia wa mali wanazomiliki, ili kuweka mazingira mazuri wanaobaki na kuepusha migogoro katika jamii inayowakosesha haki wanawake na watoto na wakati mwingine kukimbilia mitaani.

Aidha, Daudi alisema, wamekuwa wakitoa msaada wa kisheria kwa wanaohitaji kusaidiwa juu ya masuala yote ya unyanyasaji ikiwamo mirathi na ukatili wa kijinsia na miongoni mwa kesi nyingi ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara ni wanawake kutaka kuvunja ndoa na kugawana mali walizochuma ili kuepuka kunyang'anywa zote.

Hata hivyo, alisema unapoandika wosia unatakiwa kwenda kuuhifadhi katika nyumba za ibada, taasisi za kifedha, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA) au Mahakamani na wamekuwa wakitoa elimu mara kwa mara kwa wananchi kwa kushirikiana na watoa huduma ngazi za jamii na wengi wamekuwa wakitokeza kuomba msaada wa kisheria juu ya ndoa na mirathi.

Mkazi wa Busoka, Winfrida Natalisi alisema watu wengi hawana elimu ya kuandika wosia na kwenye jamii anayotoka ya kisukumu mwanaume anapokufa anarithiwa na mdogo wake, ili kuendelea mali nasio kuridhiana na hata akikataa anatakiwa kuondoka na kuacha kila kitu wakiwemo watoto aliowazaa.

# TARI, wakulima kushirikiana kuwezesha usalama wa chakula

**Na Restuta Damian,** KAGERA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Maruku imesema iko haja ya kushirikiana kwa karibu zaidi na wakulima, ili kuwawezesha namna sahihi ya upatikanaji wa chakula bora na salama na kuongeza usalama wa chakula nchini.

Hayo yamebainishwa jana na Meneja wa kituo hicho, Dk. Mpoki Shing'wera, wakati akizungumza na Nipashe katika maonesho ya Siku ya Chakula Duniani iliyohitaji kufahamu ushirikishwaji wa wakulima katika uandaaji na upatikanaji wa usalama wa chakula.

"Tunakuwa na uzalishaji wa mbegu na tunatoa nafasi kwa mkulima na hii ni kumwakikishia kwamba anapokuwa akifanya uzalishaji wake shambani anajua iko tija shambani kwake na hata sokoni anakopeleka mazao yake," alisema Dk. Shing'wera.

Alisema miaka ya nyuma watafiti walifafanua tafiti zao na kupeleka mbegu kwa mkulima, ili aweze kutumia shambani bila kujua hitaji hata pendekezo la tija ya mkulima mwenyewe tofauti na ilivyo kwa sasa.

Mtafiti kutoka kituoni hapo kitendo cha uhaulishaji wa migomba, Gabriel Luposi alisema baada ya kubaini tatizo la magonjwa katika mimea ililazimu kuingia katika teknolojia na kufanya utafiti wa zao hilo ambao utakinzana na kumpa radha ya asili mkulima.

"Kawaida wakulima wa migomba wanapenda asili ya ndizi isipotee na kwa kuona hizo tunapokea maoni yao na kuingia maabara kufanyia tafiti ya uboreshaji kwa kuunganisha aina zaidi ya moja na kupata chotara ambayo inabakia kwenye hali ya asili," alisema Lupaso.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao nchini, Nyasebwa Chimagu, alisema kwa kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inakuwa kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030, lazima kufanya mageuzi kwenye sekta ya kilimo kwa kuongeza jitihada mbalimbali.

Alisema matumizi ya pembejeo bora yanayokabiliana na upotevu wa chakula kabla na baada ya mavuno kwa kujihakikishia kuwa visumbufu vyote vinadhibitiwa na kuwa Mkoa wa Kagera umefanikiwa katika uzalishaji wa mazao yasiyo ya nafaka kwa kuwa na tani zaidi ya 700,000 huku ukiwa na asilimia 22 ya nafaka.

Hata hivyo, alisema uzalishaji wa chakula nchini kwa mwaka 2022 ulikuwa tani milioni 18 na msimu wa 2023 ulikaribia tani milioni 22 katika utoshelevu wa chakula kabla ya mwaka 2023/2024 ulikuwa asilimia 96.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 22, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 14



**Kilimo cha umwagiliaji kwa matone kinavyowapeleka mbele wakulima**

Ukurasa 12



Ubongo wa inzi unavyofanikisha kujifunza akili ya binadamu

Ukurasa 13




Sekondari Jokate inavyoakisi azma 'tokomeza ziro' Kisarawe

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# Athari za mfumo wa elimu kwa maendeleo ya akili ya watoto

BINADAMU wote ni sawa lakini akili zinajengwa na kuimarishwa kulingana na mahali wanapoishi na mazingira yanayowazunguka.

Mathalani, mtoto anayezaliwa katika taifa lenye maendeleo makubwa, ni tofauti na anayezaliwa kwenye maendeleo kidogo, ukuaji na uendelezaji akili zao, kwa kiasi utatofautiana.

Tunajiuliza, iweje tutofautiane kiakili kadri tunavyoendelea kukua hadi kuwa watu wazima? Ni kweli kuna kutofautiana katika kukua na kuendeleza akili kutegemeana na mambo kadhaa kama chakula na uhalisia wa mazingira tuliyomo.

Vilevile, jinsi tunavyolelewa pamoja na maneno tunayotamkiwa na wazazi au walezi na jamii akili za watoto zinaathirika.




Mazingira rafiki ya kujifunzia ni ufunguo wa wasomi mahiri. **PICHA: MTANDAO**

Tunatafakari unapofika umri wa kuanza shule mtoto anakuwa yupo vipi akilini? Anakwenda shuleni akibeba masuala gani akilini mwake? Walimu wanaompokea kiakili na kimaadili wakoje, wamepikwa kulingana na mahitaji ya jamii na taifa?

Ni nini matarajio ya wazazi na walezi na taifa kwa watoto wanapokuwa shuleni kujifunza ? Je, katika mifumo ya maisha ya usasa tunatarajia elimu au mafunzo shuleni yatawawezesha kuwa bora kimaisha katika jamii?

Watakuwa wakulima, wafugaji na wafanyakazi werevu wanaotoa huduma bora au ni borahuduma? Sayansi ya jamii inaonyesha kuwa mazingira yanayomzunguka mtu humuunda kiakili na kitabia.

Iwapo wanazaliwa na kukulia katika mazingira yenye ulevi uliokithiri, fujo na uovu mwingi, itakuwa vigumu kujengeka kiakili na kuwa wenye tabia nzuri. Kiuhalisia wakilelewa kwenye mazingira yaliyosheheni sauti zenye maneno na vitendo viovu watakengeuka.

Kwa upande mwingine, tunapokuwa kwenye mifumo rasmi ya elimu; ndiyo wakati muafaka wa kujijengea msingi bora na imara kwa maisha ya utu uzima ili tusichanganyike kwani ni binadamu wenye karama tofauti.

Wakati wa uhuru 1961, taifa lilitumia mfumo ya elimu wa Waingereza, baadaye liliweka mifumo iliyojengeka yenye maudhui tofauti.

Mathalani, kwa kuzingatia miongozo: uhuru na kazi, ujamaa na kujitegema, binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja. Vilevile, kwa dhana ya binadamu ni utu hivyo, thamani kubwa ya binadamu ni kuuheshimu utu wake.

Kutokana na mitazamo hiyo na masuala mengineyo kama nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko au sitapokea wala kutoa rushwa. Maudhui hayo yalijengeka kwa msingi kwamba haki ya mtu haiuzwi wala kununuliwa kwa chochote.

Kwa kuyazingatia hayo taifa likajijengea mifumo ya elimu inayoendana na mazingira halisi, hata hivyo, ukafika wakati darasa la nane likafutwa, na ilipofika 1967 ukaanzishwa mfumo wa elimu ya msingi mwisho darasa la saba.

Juhudi za kupanua elimu ya juu ziliendelea kiasi cha kufikia hatua ya kuona vyuo vilivyokuwa vinatoa mafunzo kwa ngazi za cheti (astashahada) na stashahada (diploma) kuwa vyuo vikuu.

Vyuo vilikuwa vinatoa mafundi stadi mahiri kutokana na mafunzo au ujuzi alioupata mhitimu katika fani au mafunzo husika. Mathalani, mafundi umeme, mitambo, uashi na uhunzi.

Sidhani kama kuwapo VETA sasa ni toshelezi bado kuna haja kubwa kuwapo vyuo vya kati katika mifumo ya elimu na kuwajengea uwezo Watanzania.

Serikali imedhamiria kuondoa elimu ya msingi kuishia darasa la saba ili na mfumo wa darasa la sita. Inawezekana pia ukafika wakati tukaamua kuwa elimu ya msingi imalizikie darasa la nne na kuendelea na sekondari hadi vyuo vikuu.

Kwa mageuzi kielimu ili kuwezesha vijana wengi kuyamudu maisha, kujiajiri au kuajiriwa wengine wanahitaji msingi imara. Hivyo, hatunabudi kuzingatia umuhimu na uwepo wa vyuo vya kati mahiri kwa vijana kupata mafunzo ya stadi za kazi, ngazi ya astashahada au stashahada kumwezesha mtaalamu kumudu kazi zenye kuhitaji maarifa fulani.

Mathalani, kusimamia na kuendeleza shughuli mbalimbali kwenye vyama vya wakulima na ushirika vijijini pia mijini.

Kadhalika, tunapotaka tushughulike na kilimo na ufugaji kibiashara na kuzingatia matumizi bora ya ardhi iliyotengwa kwa kilimo na ufugaji ni vyema wakulima na washauri elekezi wapatiwe mafunzo kikamilifu.

Uzoefu unaonyesha kuwapo ongezeko kubwa la wanafunzi tangu shule za msingi hadi vyuo vikuu, huku Watanzania wakizidi kuongezeka lakini kwa upande mwingine taifa likoje kuuhalisia, kuhusu miundombinu kutoa elimu inayoikusudiwa?

Hali katika shule na vyuo si rafiki kwa mtoto au vijana wengi kupata elimu bora. Pamoja idadi yao kuendelea kuongezeka mikakati endelevu kuhakikisha miundombinu inaambatana na ongezeko la wanafunzi na wanavyuo, haijazingatiwa ipasavyo. Kwa utoaji elimu iliyo bora miundombinu inamaanisha madarasa, kumbi za mihadhara, vyumba vya maabara, ofisi za walimu na wahadhiri, vyoo toshelezi, majiko, mabwalo, kumbi za mikutano, stoo, nyumba za walimu na watumishi wengine, viwanja vya michezo na mafunzo kivitendo.

Wazazi na walezi tunawajibika kutembelea shule kuona mazingira

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ubongo wa inzi unavyofanikisha kujifunza akili ya binadamu



UMEWAHI kumfikiria mdudu mfano mende na akili yake, unadhani hana akili, ukweli ni kwamba anazo tena sana.

Mathalani, kama kuna mwanga haonekani, lakini usiku taa zikizimwa wanajaa jikoni au popote penye chakula. Ikitokea ukiingia ghafla na kuwasha taa wanafahamu pa kukimbilia na kujificha usiwaue kwa urahisi. Hiyo ni akili nyingi kwa mdudu.

Mdudu nzi, naye ana akili, mfano kutembea juu ya kitu anachoona kinalika, kuelea juu na pia madume kuimba nyimbo za kuwavuta majike yote hayo yanafanywa na ubongo mdogo kuliko kichwa cha pini ya ofisini (office pin) wa inzi.

Ikumbukwe nzi huishi siku 15 hadi 30 na inategemea hali ya joto na maisha inayopitia. Ubongo mdogo lakini kazi kubwa na za kushangaza.

Wanasayansi wanaotafiti ubongo wa nzi wamegundua ulipo, umbo na mwingiliano wa kila seli moja kati ya seli 130,000 zinazoundа na viunganishi vyake milioni 50.

Mtaalamu mbobezi wa ubongo asiyehusika na utafiti huo mpya anaeleza kuwa haya ni mafanikio makubwa katika kuelewa ubongo wa binadamu au mtu kujifahamu mwenyewe.

Dk. Gregory Jefferis wa Maabara ya Utafiti wa Kimatibabu (LMB), katika Chuo Kikuu cha Cambridge, anasema kwa sasa watu hawajui jinsi mtandao wa seli za ubongo katika vichwa vyao unavyoingiliana na kila moja.

"Kuna mwingiliano gani? Ni kwa namna gani mawimbi hutiririka kupitia mfumo unaoweza kuturuhusu kuchakata taarifa ili kutambua uso wa mtu, au kusikia sauti na kugeuza maneno na kuwa mawimbi ya umeme?

"Uchoraji wa ramani ya ubongo wa inzi utafanikisha kuelewa jinsi akili zetu wenyewe zinavyofanya kazi."

Anasema kuna chembechembe za nyuro milioni kwa milioni kwenye ubongo, zaidi ya zile za nzi aliyefanyiwa utafiti. Kwa hivyo mchoro wa ubongo wa wadudu unawezaje kusaidia wanasayansi kujifunza zaidi?

Picha ambazo wanasayansi wametoa zilichapishwa katika jarida la Nature, zinaonyesha nyuzi nyuzi mithili ya wavu.

Muundo wake ndiyo unaoshikilia ufunguo wa kuelewa jinsi kiungo hicho kidogo kinavyoweza kutekeleza kazi nyingi zenye kubwa na za kimahesabu.

Kutengeneza kompyuta ya ukubwa wa mbegu ya nafaka yenye uwezo wa kazi kama ubongo wa nzi ni uwezo ambao sayansi ya sasa haijafikia.

Dk. Mala Murthy, mshiriki mwingine katika mradi huo, kutoka Chuo Kikuu cha Princeton, anasema picha hizo mpya zitaleta mabadiliko kwa wanasayansi wa mishipa ya fahamu-neva.

"Itasaidia watafiti wanaojaribu kuelewa jinsi ubongo wenye afya unavyofanya kazi. Katika siku zijazo tunatumai itawezekana kuelewa kile kinachotokea katika akili zetu."

Hayo ni maoni yanayoungwa mkono na Dk. Lucia Prieto Godino, kiongozi wa timu ya utafiti wa ubongo katika Taasisi ya Francis Crick ya London, ambaye hayuko katika timu ya watafiti wa ubongo wa nzi.

"Watafiti wamegundua mfumo wa seli wa mnyoo mwenye nyuzi nyuzi 300 na funza ambaye ana 3,000, lakini kuelewa muunganiko wa seli za mdudu mwenye nyuzi nyuzi 130,000.

Ni kazi ya kiufundi ya kushangaza ambayo inafungua njia ya kuuelewa ubongo mkubwa kama vile wa panya na labda katika miongo kadhaa ubongo wetu wenyewe."

**ILIVYOFANYIKA**

Utafiti huo ulifanywa kwa kukata vipande vipande ubongo wa nzi na kuvipiga picha kila kimoja - vipande 7,000.

Kisha timu ya Princeton ikatumia akili bandia kutoa maumbo na miunganisho ya nyuroni zote. Lakini akili bandia haikukamilisha kazi hiyo na watafiti wakilazimika kurekebisha makosa zaidi ya 3,000,000 kwa mkono.

Hii yenyewe ilikuwa safari ya kiufundi, lakini kazi ilikuwa nusu tu.

Ramani yenyewe haikuwa na maana isipokuwa kuwe na maelezo ya kazi ya kila nyuzi ya ubongo huo, anasema Dk. Philipp Schlegel, ambaye anatoka katika Maabara ya Utafiti wa Kimatibabu.

"Kuelezea nyuroni ni kama kuweka majina ya mitaa na miji, saa za kufungua namuda wa kufunga biashara, nambari za simu na maoni kwenye ramani ya google."

Dk. Schlegel anaamini ulimwengu wa sayansi ya neva utaona mfululizo wa uvumbuzi katika miaka michache ijayo kutokana na ramani hii mpya."

Ubongo wa mwanadamu ni mkubwa zaidi kuliko wa nzi, na bado hakuna teknolojia ya kunasa taarifa zote kuhusu nyaya zake.

Lakini watafiti wanaamini katika miaka 30 ijaya watawezekana kuuelewa ubongo wa binadamu wote."

Ubongo wa nzi, wanasema, ni mwanzo wa ufahamu mpya, wa kina wa jinsi akili zetu wenyewe zinavyofanya kazi.

Utafiti huo umefanywa kwa ushirikiano mkubwa wa wanasayansi wa kimataifa, na umepewa jina la FlyWire Consortium.

**BBC**

# ATHARI ZA MFUMO WA ELIMU KWA MAENDELEO YA AKILI YA WATOTO

INATOKA UK.11

yalivyo ili kubaini kama yanakidhi, wanafunzi wanapata elimu bora. Watoto wanabanana kwenye madawati kukaa chini hadi kwenye miguu ya walimu, yaani kila mahali panajaa kiasi cha mwalimu kutowafikia wanafunzi nyuma ya darasa.

Je, ni sahihi? Siyo lakini hii ndiyo hali ilivyo kwenye shule zetu maana watoto wameongezeka wakati hakuna miundombinu ya kutosheleza. Iwapo hali iko hivyo kuna hatari ya kuwaona watoto wengi shuleni lakini hawafundishwi ipasavyo.

Tanzania, inahitaji mifumo ya elimu mizuri kuwezesha vijana wote wapate elimu sahihi tangu msingi hadi vyuo vikuu. Ni jambo jema, lakini tumejiandaa vya kutosha na uhalisia wake ukoje?

Karibu vyuo vingi nchini vinadahili wanafunzi wengi na wanazuoni wanalazimika kufundisha watahiniwa 200 hadi 300 sehemu moja. Vilevile, hali halisi ilivyo kwa madarasa mengi shule za msingi namba ya walioandikishwa kuanza darasa la kwanza kwenye chumba kimoja chenye uwezo wa kutumiwa wanafunzi 45-50.

Namba hiyo humwezesha mwalimu kuimudu kazi yake barabara ikiwa ni pamoja na kutambua uwezo wa kila mwanafunzi kiasi cha kuwasaidia wenye uelewa hafifu ipasavyo.

Kwenye mijadiliano na baadhi ya wahadhiri inaonekana ni vigumu kutoa mhadhara kwa watahiniwa waliojazana sehemu moja wakaelewa .

Isitoshe baadhi ya waliosajiliwa kusomea shahada hawakidhi vigezo vinavyotakiwa hivyo hali hiyo inabaki kuwa kitendawili. Ukihoji mhadhiri kwamba unapotoa kazi ya kufanya kwa wanafunzi 200 hadi 300, unawezaje kusahihisha majibu yote kwa ufasaha na kwa kutenda haki?

Majibu yanaonyesha kuwa ni vigumu kuyapitia kwa ufasaha inavyotakiwa. Wahadhiri kadhaa wanakiri kuwa hilo linawezekana kwa wahusika kati ya 50 mpaka 70 tu zaidi ni changamoto kubwa. Hata hivyo wengi wanakiri kuwa namba muafaka ni wanafunzi 50 zaidi ya hapo ni kwenda kinyume na misingi kitaaluma. Inaelekea mmoja au wachache wakikamilisha kazi wenzake hupata majibu mitandaoni hivyo majibu karibu yanayofanana.

Nakumbuka nikisomea shahada ya kwanza miaka ya 1970s idadi ya watahiniwa ilikuwa rafiki kwa wahadhiri kumudu majukumu kikamilifu. Somo la taaluma za maendeleo (development studies) linalohusu wanafunzi karibu wote, lilichukua wanachuo kutoka fani mbalimbali, idadi ikawa kubwa ikishangaza wahadhiri.

Mmoja wa wahadhiri aliwahi kusema "namba yenu ni tishio hivyo ili niweze kukabiliana na changamoto hii, nalazimika kunywa angalau bia moja kujiweka sawa kabla ya mhadhara".

Pengine nia ya serikali ni kupata wataalamu wengi zaidi; wakati tukifanya hivyo tuwe makini ili viwango visiwe chini kutokana na kutofautiana na mifumo vyuo vikuu. Vilevile, miundombinu kwenye vyuo iwe rafiki kuwezesha wanafunzi wengi wenye sifa zinazokubalika kusomea shahada.

Kwa sasa halihalisi ya miundombinu si rafiki kutokana kumbi za mihadhara kuwa chache kuliko mahitaji. Kadhalika, maabara hazitoshelezi pia wakurufunzi na wahadhiri ni wachache.

Zipo dalili zinazoashiria kuwa baadhi ya wahitimu vyuo vikuu, uwezo wa kumudu kazi au fani walizosomea ni wa chini kiasi cha kulazimika kupewa mafunzo kazini na au 'kutemwa' na mifumo iliyopo.

Waajiri wanapenda wachapakazi mahiri siyo zaidi, hivyo nashauri ifanyike tathmini ya kina kuhusu mlundikano wanafunzi kwenye shuleni na vyuoni. Je, ni sahihi kuwepo mlundikano vyuo vikuu hususani tukizingatia mifumo na kanuni zilizowekwa ili kutoa elimu bora na siyo bora elimu.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KISARAWE

# Sekondari Jokate inavyoakisi azma 'tokomeza ziro' Kisarawe




Mkuu wa Shule ya Jokate Mwegelo, Mariam Mpunga, akitoa neno wakati wa mahafali ya kidato cha nne 2024. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

WILAYA ya Kisarawe inayopatikana mkoa wa Pwani ni maarufu kwa mengi, kwanza ni kudumisha mila kuanzia kucheza ngoma hadi kula vyakula vya asili kama kasamvu kinachochanganywa na kunde pamoja ugali wa muhogo.

Pia, wakazi hawako nyuma kwenye uzalishaji mashambani ni wakulima mahiri wa mihogo, mbaazi na karibu kila nyumba ina minazi matunda yake mahsusi kuunga vyakula.

WanaKisarawe ni wapenzi wa ngoma ya unyago, wanayochezwa mabinti wakishafikia miaka 10, mila hiyo inayowagusa watoto wadogo kwa miaka mingi ilikuwa chanzo cha wasichana kukwama kielimu, hasa baada ya kupata mimba.

Mafunzo wanayopatiwa wakati wa ngoma hizo yanaelezwa kusababisha wengi wao wajiingize kwenye ngono na kupata ujauzito wakiwa bado wadogo na kulazimika kukatisha masomo.

Ikumbukwe zama hizo hakukuwa na mpango wa kurejea shuleni kuendelea na masomo yaliyokatishwa kwa sababu mbalimbali ukiwamo ujauzito.

Leo, mambo yamebadilika kutokana na kampeni zinazofanywa na serikali na mashirika ya kiraia kupinga mila zilizopitwa na wakati kama kuwacheza watoto unyago, zimeanza kuleta mabadiliko.

Jitihada zinaanza na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Jokate Mwegelo, kwa kushirikiana na Mbunge Dk. Selemani Jafo Waziri wa Viwanda na Biashara na viongozi wa wengine wanaandaa mkakati wa kujenga sekondari ya wasichana.

Inaanza kwa moto kauli mbiu 'tokomeza zero Kisarawe". Baada ya kujengwa Sekondari ya Wasichana ya Jokate Mwegelo, ikawa chachu ya wasichana wengi kupambana na kujiendeleza kimasomo.

Kuwapo kwa shule hiyo ambayo inachukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita kutoka maeneo mbalimbali kumeiamsha jamii inayowazunguka kuwapa kipaumbele watoto wao na kuanza kuzipa mgongo mila na tamaduni zilizopitwa na wakati.

Kwasasa wazazi wengi wameanza kubadilisha utaratibu wa kuwacheza watoto wao kwa kusubiri wakihitimu elimu ya sekondari ndipo na wao wanatumia nafasi hiyo kutekeleza utamaduni huo.

Sekondari ya Jokate Mwegelo yenye wanafunzi 930 kutoka waanzilishi 86 mwaka 2021 imeendeleza kauli mbiu yake ya tokomeza zero kutokana na matokeo ya kidato cha pili, cha nne na cha sita.

Mkuu wa shule hiyo, Mariam Mpunga, anaishukuru serikali kuondoa vikwazo katika shule hiyo na kuwawezesha wanafunzi kutumia muda mwingi kwenye masomo huku wakiongeza ufaulu kwenye mitihani yao.

"Shule yetu inafanya vizuri kitaaluma katika mitihani ya kidato cha pili na cha sita kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2022, 2023 na 2024 katika mitihani ya kitaifa imefaulisha kwa asilimia 100 na hakuna daraja sifuri. Ni jambo linaloonyesha kaulimbiu ya tokomoza zero kwa vitendo ikidhihirika," anasema.

Mariam anasema tangu kuanzishwa imekuwa na ongezeko la miundombinu na leo yako mabweni 10, vyumba vya madarasa 28, maktaba moja, maabara mbili, nyumba za walimu mbili jengo la utawala moja pamoja na matundu ya vyoo 30.

Anasema wanafunzi waanzilishi wa kidato cha kwanza mwaka huu watahitimu kidato cha nne, wakijiandaa kwa mtihani wa taifa utakaofanyika mwezi ujao kuonyesha walichovuna kwa kipindi cha miaka minne.

Mpunga anaeleza kwamba licha na kuwapo kwa jitihada za kutokomeza zero kama ilivyo lengo la kuanzishwa kwa shule hiyo bado haijapata chanzo cha uhakika cha maji ya kutosha ikilinganishwa na ongezeko la wanafunzi.

Aidha, anaeleza kikwazo kingine katika shule hiyo mbali ya maji kuwa kukosa ni uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi hasa kwa vile mazingira yake ni mapori.

Nyumba bora za walimu, maabara kulingana na ongezeko la wanafunzi pamoja na gari la shule la kuhudumia na kubeba wanafunzi na wafanyakazi yanapotokea matatizo mfano ugonjwa.

"Vikwazo hivi vinavyoonekana sasa vilikuwa vikubwa zaidi, namshukuru Mbunge wa Jimbo la Kisarawe Selemani Jafo, ambaye amekuwa bega kwa bega na sisi kuvitafutia mwarobaini tunaendelea kumwomba afanikishe kuimarisha mazingira ya kufundisha na kufundishia ili ufaulu unaongezeka." Anasisitiza.

Khalfan Sika ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kisarawe, ndiye mgeni rasmi wa kwanza katika mahafali ya kidato cha nne katika shule hiyo akimwakilisha mwasisi Jokate Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake Taifa (UWT).

Akizungumza na wahitimu, wazazi na walezi wa wanafunzi anasema serikali itatatua vikwazo katika sekta ya elimu na kwamba tayari imetoa Sh. milioni 900 kumalizia bwalo, na milioni 30 kupanua maabara za shule hiyo.

Sika pia anamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kisarawe kutenga bajeti kwa ajili ya kumaliza vikwazo vilivyoko shuleni hapo.

Ofisa Elimu Sekondari ya Kisarawe Edita Fue, anawakumbusha wazazi kuzingatia malezi bora kwa wanafunzi wahitimu elimu ya sekondari dhidi ya ukatili kijinsia na vishawishi hatarishi.

Diwani wa Halmashauri ya Kisarawe Hamis Dikupatile, aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri wakati Jokate Mwegelo ikianzishwa anasema vikwazo vilivyoelezwa na mkuu wa shule hiyo vitatafutiwa ufumbuzi kwa kutengewa bajeti.

Dikupatile anasema halmashauri itapambana kuviondoa kwa kutenga bajeti ili wanafunzi wanaochaguliwa kusoma katika shule hiyo wajikite kwenye masomo zaidi na kuongeza ufaulu katika jambo analoliita la motisha kwa wasichana.

Mwanafunzi wa kidato cha nne Hadija Mrisho, anasema katika mwaka wao wa kwanza kutoa kidato cha nne kwa shule hiyo wanakwenda kuandika historia kwenye kufaulu na kudhihirisha kauli mbilu ya uanzishwaji wa shule hiyo kutokana na maandalizi mazuri waliyopata.

Mbali ya kufundishwa kwa bidii wanafunzi wa shule hiyo pia wamekuwa wakiletewa wahadhiri wa vyuo vikuu wanawake ili kuwapa uzoefu na motisha wa kufanya vizuri kwenye masomo yao na kuwaaminisha kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi na kushika nafasi mbalimbali akijiamini na kusimamia malengo yake.

Kadhalika wanafanya ziara kwenye vyuo vikuu husussani cha Dar es Salaam lengo likiwa kujifunza na kujionea wanawake wanavyosoma vyuoni na waliofanikiwa kupitia elimu na namna walivyojikwamua kutoka kwenye vikwazo vya kuharibu malengo yao.

TEKNOLOJIA

NA MAULID MMBAGA

# Kilimo cha umwagiliaji kwa matone kinavyowapeleka mbele wakulima

## •Kinadhibiti upotevu wa maji, ni mizizi pekee inayofikishiwa

TEKNOLOJIA ya umwagiliaji wa matone inayohusisha kutoboa bomba matundu madogo kulingana na mimea inayohusika ili kuimwagilia maji, ni mbinu ya kisasa zaidi ya kulinda upotevu wa maji zama hizi za mabadiliko ya tabianchi.

Ni teknolojia inayotunza maji kwa sababu inadondosha maji kwenye shina pekee na hivyo kuokoa kiasi kikubwa cha maji kisifikie maeneo yasiyo na mazao.

Mabadiliko ya tabianchi ni ajenda ya kidunia, kwa sababu ya kuathiri jamii na uchumi ikiwamo uzalishaji kwenye kilimo, kuongezeka ukame na uhaba wa maji vyote vikitatiza mazao na uoto wa asili.

Mradi wa maono ya mabadiliko kwenye mazao na udongo (VACS), unaoendeshwa katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Dodoma ni moja ya shughuli zinazowafunza wakulima teknolojia ya umwagiliaji wa matone.

Taasisi ya kuendesha mifumo ya masoko ya kilimo (AMDT), inayoelimisha na kuhamasisha wakulima na wafugaji kuzalisha kisasa, ndiyo inayosimamia mradi wa VACS.

Mratibu wa tathmini na ufuatiliaji matokeo wa AMDT, Delta Shila, akizungumza na Nipashe mkoani Manyara hivi karibuni, anasema wakulima wa Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Dodoma wanawaelimisha na kuwahamasisha kutumia umwagiliaji wa matone na mbegu bora.

Anafafanua kuwa juhudi hizo ni kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wakiendeleza kilimo cha mbaazi, khoroko na kunde.

"Kuanzia Juni hadi Septemba mwaka huu, tumewafikia wakulima zaidi ya 600 wa mikoa hii, kipaumbele ni wakulima watumee teknolojia ya umwagiliaji wa matone kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi," anasema Shila.

Anaongeza:"Tunasisitiza matumizi ya mbegu bora ili kuongeza tija katika uzalishaji na kupata manufaa ya kile wanachokifanya."

Anaeleza kuwa wanahamasishwa kumwagilia kwa matone ili waendelee kuzalisha hata kama siyo msimu wa mvua.



Ofisa ugani wa Kijiji cha Gedamar, Laizer Sulle (kulia), akimwelekeza mkulima, Fatuma Iddi, namna ya kuzingatia anapolima kisasa. **PICHA: MAULID MMBAGA**

### MAFANIKIO

Wakulima waliofikiwa na mradi huo katika mikoa hiyo minne wanaelezea mafanikio ya elimu hiyo kwenye kuzalisha mazao mbalimbali, kwa mfano;

Dodo Matambo kutoka Kijiji cha Gedamar mkoani Manyara, anazalisha magunia matano ya mikunde kwenye ekari badala ya moja alilokuwa anavuna kabla ya mafunzo ya VACS.

Pia, anasema mavuno anayoyapata yanamsaidia kuinua uchumi wake hali inayomwezesha kuongeza wigo katika kilimo na kumudu gharama mbalimbali za uendeshaji wa maisha kama kusomesha watoto na kuboresha makazi yake.

Matambo anasema: "Awali milo miwili ilikuwa shida kwangu lakini sasa njaa naisikilizia kwa majirani, hiki kilimo kina manufaa kwasababu unavuna awamu nne mpaka tano kwa mwaka tofauti na ukulima waliokuwa wanafanya zamani."

Changamoto ya ukame ilisababisha kuvuna mara moja lakini umwagiliaji unawezesha kuvuna zaidi, anasema Matambo, anayetoa wito kwa wakulima wengine kuacha kuhofia gharama badala yake waachane na kilimo cha mazoea na watumie teknolojia ya umwagiliaji, mbegu za kisasa na kufuata maelekezo ya kitaalamu.

Fatuma Iddi, ni mnufaika kutoka Gedamar, ambaye kupitia mradi wa VACS, anayajua masuala muhimu ya kuzingatia kufanikisha kilimo chenye tija na kuvuna kwa uhakika.

Ozinieli Benego, kutoka kikundi cha wakulima wa umwagiliaji, Mkoka mkoani Dodoma, anasema kutokana na uhaba wa maji awali walikuwa wanalima sehemu ndogo kuzalisha mazao yasiyotosheleza familia wala ziada ya kuuza.

Anasema baada ya kukutana na AMDT wamepatiwa elimu ya namna ya kuendesha kilimo cha kisasa kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuchimbiwa visima pamoja na kuwekewa miundombinu ya sola, hatua ambayo imebadilisha mifumo ya kilimo kwa wananchi.

"Awali tulianza kulima ekari moja mpaka tano lakini mwaka jana baada ya kupata miundombinu tunalima hadi 25, na mwaka huu kutokana na kupata mifumo ya umwagiliaji kwa matone tumeongeza eneo zaidi hadi kufikia ekari 41 kwa kuwa teknolojia hiyo inatusaidia kwenye matumizi bora ya maji," anasema Benego.

Anabainisha kuwa baada ya kupatiwa mafunzo na kufuata kanuni zote za uzalishaji sasa hivi wanapata mazao kuanzia kunia tano hadi nane kwa ekari, tofauti na awali kilimo cha mazoea ambako wakipata sana hazizidi gunia mbili.

Anawashauri wakulima wengine kushiriki kilimo cha umwagiliaji kwa vile ni cha uhakika kwasababu hatua zote ikiwamo kulima, kupalilia, na mmea kupata maji zinafanyika kwa wakati na kwa usahihi.

"Kulima kwa kutegemea mvua kuna changamoto mbili mvua kuwa kubwa na kuzidi kiwango lakini pia kupungua tofauti na kiasi kinachohitaji, unalima kwa kubahatisha.

"Lakini kilimo cha umwagiliaji kinakupa uhakika mmea ukitaka maji unapata hata kama kuna jua kali tena kwa wakati, hata ukaguzi wake unakuwa ni rahisi, pia ratiba ya kupalilia inakuwa ni maalum," anasema Benego.

Oska Mashoke, mkazi wa Kijiji cha Mikongani, mkoa wa Arusha, anasema amepata manufaa zaidi ya kujua kuzalisha mbegu ya choroko na kwamba awali walikuwa hawajua kuwa zinachukua muda gani hadi kukomaa.

Anasema baada ya kupatiwa elimu ya kulima kisasa kwa mfumo wa umwagiliaji ndani ya siku 60 au miezi miwili wanaweza kuvuna, akieleza kuwa zao hilo ni mahususi kwa chakula na biashara.

"Hizi mbegu walizotuletea ni bora na za kitaalamu tofauti na zile tulizokuwa tunavuna zilisababisha kuwa na uzao mdogo," anasema Mashoke na kuongeza kuwa,

Elimu waliyopatiwa kupitia mradi wa VACS imeinua uzalishaji kwa kufuata kanuni bora za kuotesha kitaalamu, kupalilia na kumwagilia wakiongeza uzalishaji kutoka gunia moja na nusu mpaka sita kwa ekari.

### SULUHU YA KUDUMU

Katika hatua nyingine, Ofisa Kilimo wa Kijiji cha Gedamar, Laizer Sulle, anasema wanaufurahia mradi wa VACS kwasababu unatoa suluhu ya changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kama ukame na mvua kutokunyesha kwa wakati.

Anasema kilimo cha umwagiliaji kwa matone kinawahakikishia wakulima usalama wa chakula, na kwamba vyakula ambavyo vilikuwa vinapatikana kwa msimu sasa vipo wakati wote kwasababu teknolojia inayotumika ni tofauti na ya kilimo cha mazoea.

"Mfumo huu wa umwagiliaji kwa matone ukishauweka shambani unaendelea na mambo mengine, utakachotakiwa kufanya ni kufunga au kufungua maji, huku ukijua kwamba baada ya muda fulani mimea imeshapata maji ya kutosha." Anasema Sulle.

Mkurugenzi wa AMDT, Charles Ogutu, anasema teknolojia hiyo ya umwagiliaji itaendeleza kilimo nchini, akisisitiza kuwa sekta ya kilimo itabaki kuwa mama na kwamba inahitaji wataalamu na wadau wengi kuiendeleza.





## Serikali yaahidi kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuweka misingi mizuri ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mkurugenzi Msaidizi, Sekta ya Uchumi na Uzalishaji kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Enock Nyanda, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifunga kongamano la mwaka la wadau wa mazingira lililoandaliwa na Forum CCC kwa kushirikiana na wadau kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali.

Nyanda alisema athari za mabadiliko ya tabianchi ni kubwa, hivyo zinahitajika juhudi za pamoja katika kukabiliana na hali hiyo.

Alieleza kuwa TAMISEMI kama wadau wamekuwa wakiratibu idara za kisekta, taasisi za serikali, kilimo, mifugo, maji ili kukabiliana na mabadiliko hayo.

Aidha, aliwataka wadau hao kuunga mkono jitihada za serikali za kuitaka jamii kutumia nishati safi za kupikia kwa sababu inaokoa uharibu wa mazingira na kuimarisha afya za watu.

Alisema kuna umuhimu kwa serikali, wadau wa maendeleo kuangalia namna ya kufadhili mashirika na vikundi vinavyotoa elimu, ili jamii nyingi athari za mabadiliko ya tabia nchi na kuchukua hatua.

Naye Mshiriki wa kongamano hilo, Mariethа Mnazo kutoka Shirika la Wanawake na Watoto la Ifakara, alisema waathirika wakubwa wa athari za mabadiliko ya tabia nchi ni wanawake na elimu zaidi inatakiwa kutolewa ili kujua mbinu za kukabiliana na hali hiyo.

**TAMISEMI kama wadau wamekuwa wakiratibu idara za kisekta, taasisi za serikali, kilimo, mifugo, maji ili kukabiliana na mabadiliko hayo.**

# Polisi wachunguza jinai kifo mkazi Bahi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JESHI la Polisi kwa kushirikiana na wataalamu wengine limeanza kuchunguza kama kuna jinai kwenye kifo cha Mkazi wa Chipanga A, Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Lucia Iramba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Msemaji wa Jeshi hilo, David Misime, jeshi hilo lilipokea maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Rebeca Nsema, Oktoba 15, mwaka huu juu ya kifo hicho kilichotokea Septemba 25, mwaka huu kwa kujinyonga.

Alisema ili kupata ukweli wa taarifa zilizotolewa baada ya uchunguzi wa awali, jeshi hilo ambalo lina jukumu la kufanya upelelezi wa matukio ya kujinyonga litashirikiana na wataalamu wengine wa kuchunguza matukio ya vifo.

"Uchunguzi huu ni wa kuona kama kuna jambo la jinai ambalo uchunguzi wa awali haukuweza kulibaini," alisema.

Alitoa wito kwa mwananchi mwenye ukweli wa jambo lolote linalohusu tukio hilo kujitokeza, ili kupata ukweli na kwamba jeshi hilo halitasita kuchukua hatua kulingana na sheria za nchi.

Hivi karibuni, katika ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi, Mkuu wa Wilaya hiyo alionesha kuchukizwa na utendaji kazi wa baadhi ya watumishi wa serikali kwenye kijiji hicho kutokana na wananchi kuonesha kuwapo kwa utata wa kifo hicho.

Mkuu huyo alisema kuna watumishi (Polisi Kata na Mganga wa Kituo ch Afya) wanadaiwa kuficha ushahidi wa kifo hicho.

Akizungumza na wananchi hao, Mkuu wa Wilaya Nsema alisema "Wananchi wanalalamika wana mashaka na kifo, lakini vyombo vinavyohusika wataalamu wako hawakupi taarifa kwa wakati na kuhoji alikaguaje mwili bila kuwa na fomu husika? Nani alimruhusu kwenda kuchunguza? Niliuliza ulithibitishaje amejinyonga?"

Nsema alidai kuwa kwa mujibu wa wananchi mkazi huyo alikuwa na ugomvi na hawara wa mume wake.



Waziri wa Madini ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde (kushoto), akipokea tuzo ya utumishi uliotukuka wa kutatua kero za wananchi wakiwamo wachimbaji wadogo wa madini, kutoka kwa Askofu Mkuu wa Kanisa la Karmeli Assemblies of God, Dk. Evance Chande (kulia) na Askofu Mkuu wa Kanisa la Harvest Gospel Mission, Benjamin Mwinula (wa pili kulia), baada ya kuzungumza na waumini mbalimbali waliohudhuria mkutano wa Neno la Mungu uliofanyika Ipagala Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali kuongeza afua za kutokomeza malaria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge na Masuala ya Ukimwi imeshauri serikali kuongeza afua za kutokomeza ugonjwa wa malaria katika mikoa inayoongoza kwa maambukizi ya ugonjwa huo ikiwamo Tabora.

Mwenyekiti wa kikao cha kamati hiyo, Bernadeta Mushashu alitoa rai hiyo jana kwenye kikao cha kupokea taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu ugonjwa huo.

Alisema pamoja na jitihada zilizofanywa na serikali na kuonesha mafanikio kwenye mikoa mbalimbali, ni vyema afua zaidi ziongezwe kwa mikoa ya Tabora ambao unaoongoza kwa asilimia 23.4, Mtwara kwa asilimia 20, Kagera asilimia 18, Shinyanga asilimia 16 na Mara asilimia 15.

"Tunaipongeza serikali kwa juhudi na malengo ya kuendelea kutekeleza afua za kutokomeza malaria pamoja na kufanikiwa kupunguza mpaka chini ya asilimia katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Singida, Iringa, Songwe, Dar es Salaam na Mwanza," alisema.

Alitoa rai kwa wananchi kuendelea kutekeleza ushauri wa madaktari kuhusu matumizi sahihi ya vyandarua pamoja na kuweka mazingira yanayowazunguka safi na salama ili kuzuia mazalia ya viluilui vya mbu.

Awali, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema jitihada zinazochukuliwa na Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP), kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na wadau wa sekta ya afya zimewezesha kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo kupungua kutoka asilimia 14.8 ya mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8.1 mwaka 2022.

Alitaja jitihada hizo ambazo zimefanywa ni pamoja na kutekeleza mikakati ya udhibiti wa mbu wa malaria kwa njia ya utengamano.

Pia alisema ugunduzi, matibabu na tiba kinga dhidi ya malaria imewezesha mafanikio hayo kwa takribani miaka nane na kupunguza wagonjwa wa malaria wanaotibiwa kama wagonjwa wa nje (OPD) kwa asilimia 55.

"Serikali imetekeleza afua mbalimbali kwa takribani miaka minane na kufanikiwa kupunguza kiwango cha malaria kwa asilimia 45 kutoka 14.8 hadi 8.1 pamoja na kupunguza wagonjwa wa nje kwa asilimia 55 ambapo awali walikuwa ni milioni 7.7 hadi milioni 3.5 kwa mwaka 2023,"alisema.

Dk. Mollel alisema kuwa kwa sasa mpango wa taifa wa kudhibiti malaria unatekeleza mpango mkakati wa sita wa mwaka 2021 mpaka 2025, wenye lengo la kupunguza kiwango cha chini kutoka asilimia 7.5 hadi 3.5 ifikapo 2025.





# Moto wateketeza madarasa, ofisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MOTO ambao chanzo chake bado hakijafahamika, umeteketeza vyumba vitatu vya madarasa na ofisi ya mwalimu katika Shule ya Msingi Jitegemee iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya.

Moto huo ulizuka juzi asubuhi wakati wananchi wakijiandaa kwenda kanisani huku wengine wakielekea kwenye vituo vya kujiandikisha kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mlima Reli iliko shule hiyo, Malongo Sumuni alisema alikuwa anashirikiana na mabalozi na viongozi wengine kuhamasisha wananchi kwenda kujiandikisha ndipo akapigiwa simu kuwa shule inaungua.

Alisema alipofika shuleni hapo alikuta moshi umetanda madarasa yote matatu na Ofisi ya Mwalimu Mkuu ndipo wakaanza kushirikiana na wananchi kuukabili kwa kuchota maji na kumwagilia hali ambayo ilisaidia kuupunguza kasi.

Alisema mbali na kuuzima moto huo pia baadhi ya wananchi walivunja madirisha ya vyumba vya madarasa vilivyoko jirani na kuanza kutoa madawati na samani zingine zilizokuwamo ili visiungue endapo moto ungelifikia.

Alisema wakati wanaendelea kukabiliana na moto huo waliwasiliana na Jeshi la Zima Moto na Uokoaji na Polisi kwa ajili ya kuomba msaada wa kuuzima moto huo.

"Tunawashukuru Jeshi la Polisi na Zimamoto wameitikia wito haraka na kuja kutusaidia, wameleta magari mawili ya maji ambayo ndiyo yaliyosaidia kuuzima kabisa moto huu, lakini madarasa yameungua na vyote vilivyokuwamo," alisema Sumuni.

Balozi wa Mtaa huo, Zakaria Kayoko alisema alikuwa yuko mtaani kuhamasisha wananchi kwenda kujiandikisha kwa sababu ilikuwa ndiyo siku ya mwisho na ndipo akaambiwa na mwananchi mmoja kwamba shule inaungua.

Alisema baada ya kufika shuleni alikuta kweli moto unawaka ndipo akatumia kipaza sauti alichokuwa anakitumia kuhamasisha wananchi akaanza kuwatangazia kuhusu dharura hiyo na ndipo wananchi wakakusanyika na kuanza kuuzima.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Justine Kessy, alisema vyumba viwili vya madarasa na ofisi yake viliteketea pamoja na mali zote zilizokuwamo isipokuwa chumba kimoja samani zake zilipona kiasi baada ya moto huo kudhibitiwa.

Alisema kwenye ofisi yake nyaraka mbalimbali za serikali zilizokuwamo zimeteketea vikiwamo vyeti vya wanafunzi, barua na nyaraka zingine muhimu zinazoihusu shule hiyo.

"Kwenye ofisi yangu hakijaokolewa chochote, mali zote zilizokuwamo zimeteketea na kwa sasa hatuwezi kujua thamani halisi ya mali hizo mpaka nitakapotuliza kichwa na kuanza kukumbuka kimoja kimoja," alisema Mwalimu Kessy.

Diwani wa Kata ya Utengule-Usongwe, Yona Ntunjilwa, aliwashukuru wananchi wa mtaa huo kwa mwitikio walioonyesha kwenye tukio hilo akidai kuwa wasingewahi huenda madarasa yote yangeteketea.

Aidha, aliwashukuru pia maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na wa Jeshi la Polisi kwa kuitikia wito wa wananchi wa eneo hilo akidai kuwa wasingewahi hali ingekuwa mbaya zaidi.

"Ni kweli moto huu umesababisha hasara lakini tunaweza kusema ni bora umetokea leo (juzi) jumapili wakati watoto wakiwa nyumbani, ungezuka siku ya shule huenda tungekuwa tunazungumza jambo lingine," alisema Ntunjilwa.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na uokoaji Mkoa wa Mbeya, Malumbo Ngata alisema walipokea simu kutoka kwa mmoja wa wananchi akieleza kuwa kuna ajali ya moto shuleni hapo na wanaomba msaada wa kuukabili.

Alisema waliondoka haraka ofsini kwenda kuuzima moto huo wakiwa na magari mawili ambayo mojawapo linafanya kazi kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) na kwamba walipofika walianza kuukabili moto huo na wakafanikiwa kuudhibiti.

Aidha, alisema chanzo cha moto huo bado hakijabainika lakini wanahisi inaweza ikawa ni hitilafu ya umeme.



Maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, wakisikiliza maelezo kutoka kwa mmoja wa wananchi wa Mtaa wa Mlima Reli katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuhusu ajali ya moto iliyoteketeza vyumba vitatu na ofisi ya mwalimu mkuu katika Shule ya Msingi Jitegemee. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Asilimia 46 watumia njia zisizo rasmi kutunza fedha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 46 ya Watanzania wanadaiwa kuwa wanatumia njia zisizokuwa rasmi kutunza fedha zao hali ambayo inakwamisha maendeleo ya nchi pamoja na kuhatarisha usalama wa fedha zao pamoja na maisha.

Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha wa Hazina, Janeth Hiza aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya wiki ya huduma za fedha ambayo kitaifa yanafanyika mkoani humo.

Alisema utafiti huo wa Fin Scope Survey ulifanyika mwaka 2023 na kwamba hali hiyo ndiyo iliyoilazimu serikali kuandaa maadhimisho hayo, ambayo yatatumika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia huduma hizo.

Alisema maadhimisho hayo yanatarajiwa kuzinduliwa rasmi leo na Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko na kuendelea kwa muda wa wiki nzima ambapo wadau mbalimbali wa huduma za fedha watakuwa wanatoa nelimu kwa wananchi.

"Kuna baadhi ya watu wanaamini kwamba tunapozungumzia huduma za kifedha basi ni kuhifadhi fedha pekee, hata kujua namna sahihi ya kutunza fedha zako, matumizi na namna ya kuweka akiba," alisema Janeth.

Aliwataka Watanzania kuwa na utamaduni wa kutumia nia rasmi za kifedha kufanya shughuli zao, ili kuimarisha usalama wa fedha zao na kuimarisha usalama wa maisha yao.

Aidha, alisema katika maonyesho hayo zitakuwapo taasisi mbalimbali za kifedha kwa ajili ya kutoa elimu, kampuni za bima kwa ajili ya kutoa elimu ya bima mbalimbali zikiwemo za nyumba vyombo vya moto fedha pamoja na bima za maisha.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha kwamba mpaka kufikia mwaka 2025 Watanzania wanaotumia huduma hizo rasmi wawe wamefikia asilimia 80.

Baadhi ya wadau wa huduma za fedha wanaoshiriki maadhimisho hayo, walisema utaratibu huo utawasaidia Watanzania wengi kupata elimu na kuboresha hali ya matumizi ya huduma hizo.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Mamlaka ya masoko, mitaji na dhamana (CMSA), Stela Anastaz, alisema watayatumia maadhimisho hayo kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kuwekeza kwenye masoko mbalimbali yakiwamo ya hisa.

Alisema watanzania wanaotunza fedha zao ndani ama kwa nji zingine zisizokuwa rasmi huwa hawawezi kupata maendeleo kutokana na fedha zao kutozaa na hivyo akawataka wananchi kutumia njia rasmi ili wajipatie maendeleo.

## Tume yaanza kupima ardhi mipaka vijiji 14

**Na Nebati Msokwa,** RUNGWE

TUME ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeanza kupima upya mipaka ya vijiji 14 katika kata nne za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo wilayani Rungwe, kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi wa vijiji hivyo na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Meneja wa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi Kanda ya Kusini, Pili Msati, alisema kazi hiyo ya upimani wa ardhi kwenye vijiji hivyo inafanyika kupitia Mradi wa Uboreshaji na Usalama wa Miliki ambao unalenga kuwasaidia wananchi kuwa na matumizi bora ya ardhi.

Alisema wananchi watakaonufaika na mradi huo wilayani Rungwe watasaidiwa kupanga matumizi ya ardhi yao pamoja na kuainisha mipaka ya maeneo yao, ili kumaliza migogoro ya ardhi waliyonayo.

Maofisa Watendaji wa Vijiji vya Mwela na Kilasi vilivyoko Kata za Kandete na Luteba walisema zoezi hilo litakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi, ambao sasa wataanza kutumia ardhi yao kwa kuzingatia shughuli zao za kiuchumi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mwela, Pendo Mwasajile, alisema mradhi huo ukikamilika utawasaidia wananchi kujua maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za kilimo, ufugaji na hata biashara hali ambayo itaondoa migogoro miongoni mwao.



## Mbunge: Wanaotamani Muungano uvunjike watathmini hasara yake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wanasiasa wenye fikra ya kutaka Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uvunjike wametakiwa kwanza wapime na kujua gharama za jambo hilo.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Wanawake, Khadija Hassan Aboud, aliyasema hayo visiwani Zanzibar, wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu masuala ya siasa na Muungano.

Alisema isiwe rahisi mtu kutamka Muungano uvunjike bila kujua viwango vya madhara na hasara zitakazoikumba jamii.

Khadija alisema ni vyema pande mbili kwa nchi wanachama ziendeleze utashi wa kuzumgumzia kuondoa changamoto zilizoko zinazolalamikiwa na wananchi na kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

Alisema si vyema kwa viongozi wa kisiasa bila kupima wakafikia uamuzi wa kutoa matamshi yanayojenga hofu kwa wananchi.

Aidha alisema viongozi dhamana wa serikali mbili si vyema wakawa wanakutana katika majadiliano mezani wakijajadili changamoto hizo kila wakati bila kufikia tamati.

"Uamuzi wa kuvunja muungano ni kubwa kuliko inavyofikiriwa na baadhi ya wanasiasa na vyama vyao. Wanaotaka kuvunja muungano wamepima na kujua faida na athari zake ?" alisema Khadija.

Aidha, alisema kuvunja muungano wenye umri mkubwa kama wa Tanganyika na Zanzibar, si jambo jepesi na yanaweza kutokea mambo makubwa yasiotazamiwa na jamii.

"Muungano huu umeleta manufaa makubwa kuliko hasara na changamoto zinazozungumziwa. Muungano umebeba maisha ya watu, mali zao,vitega uchumi na rasilimali kadhaa," alieleza mbunge huyo.

Pia alisema mawazo ya kuvunja muungano pamoja na kwamba hayakubaliki chini ya sera ya CCM, viongozi hawajakata tamaa kutafuta ufumbuzi wa kurekebisha yote yanayolalamikiwa.

"Wanasiasa tusichezee maisha ya watu. Kutamka maneno ya kutaka kiongozi ushangiliwe kuna gharama yake. Lazima tutafakari pamoja na kufikia tamati kwa njia za kujenga kuliko kubomoa," alisema Khadija.

**Wanasiasa tusichezee maisha ya watu. Kutamka maneno ya kutaka kiongozi ushangiliwe kuna gharama yake. Lazima tutafakari pamoja na kufikia tamati kwa njia za kujenga kuliko kubomoa.**



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga (kulia), akiwahudumia watalii katika maonesho ya chakula cha asili kinachotokana na kilimo hai katika shamba la kilimo hai la Msonge huko Shakani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kilimo cha mseto chaongeza mavuno

**Na Rahma Suleiman aliyekuwa**

**MUHEZA**

KILIMO mseto kimewasaidia wakulima wa Tarafa ya Amani, Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga kuimarisha mimea shambani na kupata mavuno zaidi hasa kwa zao la karafuu.

Hayo yalisemwa na wananchi wa tarafa hiyo wakati wakizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliofika katika wilaya hiyo kwa ajili ya ziara maalumu ya kimafunzo katika kuangalia maendeleo yaliyopatikana baada ya ujio wa utekelezaji wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Nipael Sabuni ni miongoni mwa wakazi wa Kijiji cha Kwezitu katika Tarafa ya Amani, alisema kilimo hicho kimesaidia utunzaji wa mazingira na hata wale wanyama ambao walitoweka hivi sasa wameanza kurejea katika kijiji hicho wakiwamo Mbega.

"Jinsi ya kutunza mazingira yetu itasaidia sana watoto wetu kunufaika baadaye kwa sababu kuna wanyama ambao mimi sikuwahi kuwaona kijijini kwetu, lakini nimewaona hivi sasa baada ya kutunza mazingira yetu na kumwona mnyama anayeitwa mbega," alisema.

**Hivi sasa hali ya hewa ni nzuri, ile hali ya ukame imeanza kuondoka na tumekuwa tukipata mvua za wastani na hali ya kilimo imeimarika.**

Alisema kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili wamepewa elimu jinsi ya njia za wanyama na kutoka kujua kanuni za ushoroba na kutokata miti ovyo ambapo kumewaimarishia thamani ya misitu.

Alisema pia wamefundishwa kilimo mseto ambacho kimesaidia kurutubisha uoto wa ardhi na kunufaika na kilimo hicho kwa kupata mazao ya chakula na biashara ikiwamo zao la karafuu, mdalasini, pilipili manga, hiliki, maharage na mahindi.

Alisema awali kabla ya mradi huo, mazingira na vyanzo vya maji havikuwa salama, lakini wamewekewa vibao elekezi ambavyo vinatoa ujumbe sahihi wa uhifadhi mazingira na sasa vyanzo vya maji vipo vizuri pamoja na uwepo wa miti ya kutosha kijijini hapo.

Mwenyekiti wa kijiji cha Kazita, William Hiza alisema elimu waliyopatiwa kuhusu uhifadhi wa mazingira imesaidia kurejesha uoto wa asili kijijini hapo na hivi sasa wananchi wanaelimu ya kuandaa mashamba ikiwemo kuweka mifereji ya makinga maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.

"Hivi sasa hali ya hewa ni nzuri, ile hali ya ukame imeanza kuondoka na tumekuwa tukipata mvua za wastani na hali ya kilimo imeimarika," alisema Mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, alisema yeye ni mnufaika mkubwa wa kilimo mseto hasa kwa mazao ya viungo ikiwemo karafuu ambapo kimemuwezesha kujenga nyumba ya makazi kutokana na zao hilo.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kwezitu, Esther David Kiliwa, alisema mradi huo umeleta mabadiliko makubwa katika vijiji vilivyoko kwenye ushoroba wa Amani-Niro na vijana wamenuafaika na kilimo baada ya ardhi kuwa na matumizi bora.

Alisema mradi wa kilimo hai kupitia Shirika la GFP Organics wamewasaidia wananchi wakiwamo vijana kupata fursa ya kutengeneza miche ya miti mbalimbali na sasa wanawahamasisha wananchi kulima kilimo hai na kilimo mseto ambacho kinamanufaa makubwa.

Ofisa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Issa Msumari, alisema wameunda kamati za matumizi bora ya ardhi katika halmashauri hiyo, ili kuweka uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## HABARI KITAIFA




Mfanyabiashara mdogo katika soko la Mbagala Charambe, Dar es Salaam, aliyejitambulisha kwa jina la Fatuma Mwinyi, akielezea madhara ya rushwa ya ngono, wakati Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), lilipofika sokoni hapo jana, kuendesha kampeni ya kupiga vita rushwa ya ngono iitwayo 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Asisitiza miradi taka sifuri ifike mitaani

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI zinazotekeleza miradi ya taka sifuri zimesisitizwa kupeleka miradi hiyo katika ngazi ya mitaa, ili kupunguza idadi ya taka zinazopelekwa dampo ambazo nyingi hutupwa ovyo mitaani.

Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi wa Taka na Usafi wa Mazingira cha Jiji la Dar es Salaam, Philipo Beno, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua mradi wa taka sifuri katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Jangwani unaosimamiwa na Shirika la Mazingira Plus.

Alisema kwa sasa Jiji la Dar es Salaam tani 1320 kwa siku, kati ya hizo ni asilimia 6.5 pekee ndio zinarejeshwa, na kuwa na idadi kubwa ya taka zinazopelekwa dampo na nyingine hutupwa ovyo mitaani.

Aidha, alisema miradi hiyo ikipelekwa kwa wananchi wa kawaida katika ngazi ya mitaa itakuwa msaada mkubwa wadhibiti taka nyingi kupelekwa kwenye madampo ambayo nayo yamezidiwa na wingi wa taka.

"Halmashauri ya Jiji la Ilala kwa siku wanazalisha tani 1,320 za taka hiyo ni kwa siku, taka hizi zote zinatakiwa zitolewe na kupelekwa dampo, tukikaa vizuri na taka sifuri suala hili likashuka chini kwa jamii tukafanya utaratibu wa kutenganisha taka ambapo kufanya hivyo litachukua taka chache," alisema Beno.

Alisema Halmashauri ya Ilala imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutenganisha taka hatarishi za hospitalini na nguvu kama hiyo pia inahitajika katika utenganishwaji wa taka za nyumbani.

Alisema mradi wa taka sifuri shuleni utasaidia wanafunzi na walimu kwa kuwa elimu hiyo wataipeleka katika jamii na kuanza kutenganisha taka.

"Mradi huu wa taka sifuri shuleni unasaidia kutengeneza jamii ya vijana itakayoleta mapinduzi katika utunzaji wa taka, pia kupitia taka hizi tutafaidika kwa kupata mbolea mbalimbali," alisema Beno.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mazingira katika Taasisi ya Mazingira Plus, Ramadhani Mwakae, alisema shule hiyo ni ya pili kukabidhiwa mradi wa taka sifuri na kuitaja shule ya kwanza kukabidhi ni Sekondari ya Kibasila iliyoko Wilaya ya Temeke.

Alisema watakabidhi mradi kama huo katika Shule ya Sekondari ya Dar es Salaam iliyoko wilaya ya Ilala na matarajio yao ni kukabidhi miradi hiyo kwa shule zote za sekondari na msingi nchini.

"Dhumuni la mradi huu ni kupambana na mabadiliko ya tabia nchi hususani kudhibiti uchafuzi wa taka shuleni lakini, pia malengo ya mradi huu ni kufanya uchechemuzi wa sera na kuishauri serikali kusimamia utekelezaji wa sera," alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha tatizo la mabadiliko ya tabia nchi ni la kimazingira hasa plastiki na taka ozo na kuyasihi mashirika yasiyo ya kiserikali yaungane nao katika kampeni hiyo ili ifikapo 2030 jamii itengeneze mtandao wa taka sifuri.

Mwakilishi wa Taasisi ya Kimataifa ya Nagu, iliyofadhili mradi huo, Dorothee Braun, aliipongeza Mazingira Plus kwa kubuni mradi huo utakaoleta mabadiliko makubwa katika uhifadhi wa mazingira.

# Mavunde aagiza kufungwa GPS magari ya maofisa madini

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ameagiza kufungwa mfumo wa GPS kufuatilia magari mapya 25 yaliyotolewa kwa maofisa madini wa mkoa ili yafanye kazi iliyokusudiwa na kusaidia kufikia lengo la makusanyo ya Sh. trilioni moja kwa mwaka 2024/25.

Akizungumza jana jijini hapa wakati wa hafla ya kugawa magari hayo ambayo ni kati ya magari 89 yaliyoagizwa na Tume ya Madini, Mavunde alisema vitendea kazi hivyo vinapaswa kutumika kurahisisha utendaji kazi wa maofisa hao, kuimarisha ukusanyaji maduhuli na kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

"Tuna malengo yetu tumejiwekea ya kuingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali fedha za kutosha katika sekta hii ya madini. Mwaka 2015/16 sekta ya madini iliingiza katika mfuko huo Sh. bilioni 161 na mwaka 2024/25 tumewekewa lengo kuingiza makusanyo ya Sh. trilioni moja," alisema.

Waziri Mavunde alisema makusanyo ya siku 90 (Julai-Septemba) yanadhihirisha malengo hayo yatatimia ambapo waliweka malengo ya kukusanya Sh. bilioni 249 na hadi sasa wamekusanya zaidi ya Sh. bilioni 287 na kuvuka lengo kwa asilimia 106.

"Hivyo, kwa vitendea kazi hivi maana yake vinakwenda kuimarisha zoezi zima la kazi za kila siku za Tume ya Madini kusaidia kwenye ufuatiliaji na kuongeza makusanyo yetu na kuziba mianya inayosababisha kukosekana kwa mapato," alisema.

Aliongeza kuwa maofisa madini hao walikuwa wanafanya kazi kwenye mazingira yasiyo rafiki na kwa sasa kwa kupatikana kwa magari hayo hawatakuwa na kisingizio.

"Magari haya yakatumike kwa kazi iliyokusudiwa nimeshatoa maelekezo kwa Katibu Mkuu, tunayafunga magari yote GPS, ili kuwa na uwezo wa kuyaona tukiwa Makao Makuu na kazi yanayofanya kwa maana ya mizunguko, niwaambie mapema kabisa ndugu zangu Maofisa Madini wa Mikoa ni magari ambayo tutaangalia na kazi yanayofanya hatutegemei yaende kukaa au kutumika kwenye shughuli ambayo si ya msingi ya wizara," alisema.

Waziri huyo alisema magari hayo yanakwenda kuimarisha sekta ya madini na kuwataka maofisa na watumishi wa kuhakikisha inatoa mchango chanya katika ustawi wa uchumi wa Tanzania.

"Mwaka 2017 baada ya kufanyika marekebisho ya sheria yalipeleka kuundwa kwa Tume ya Madini na ilipewa jukumu la kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kupitia sekta ya madini kwa kipindi cha muda mrefu Watanzania imekuwa ni shauku yao kuona sekta inachangia ukuaji wa uchumi wa nchi,"alisema.

Alieleza kuwa sekta hiyo ni miongoni mwa sekta chache ambazo zinaangaliwa katika kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi.

"Rais Samia ameendelea kuiboresha na kuiimarisha Wizara ya Madini kupitia ongezeko kubwa la bajeti ambalo limetufanya kwa sasa tuwe na urahisi wa kutekeleza majukumu yetu, bajeti ya Wizara ya Madini imeongezeka kutoka Sh.bilioni 89 kwa mwaka 2023/24 hadi Sh.bilioni 231 kwa mwaka 2024/25,"alisema.

Awali Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Ramadhani Lwamo, alisema Sh. bilioni 18 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 89 na pikipiki 140.

"Magari haya 25 yanayokabidhiwa leo ni awamu ya kwanza kati ya 89 ambayo Tume itayapata kwa ajili ya ukusanyaji wa maduhuli, ni matunda ya jitihada za wizara kuhakikisha wizara inakuwa na vitendea kazi vya kutosha ili kutekeleza majukumu yake," alisema.

**SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 89/2024**

**SWALEHE KASANDA ..........................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**AMINA MILANZI ....................................MJIBU MAOMBI**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 04/11/2024 saa 6:00 mchana. Shauri linakuja kwa ajili ya kutajwa.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo name na muhuri wa baraza hili leo tarehe 17/09/2024.

MWENYEKITI

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)

SONGEA

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA TANZANIA

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**Annania Zachalia Miligo** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 624 DSV** yenye jina la China Road and Bridge Corporation (T) Ltd. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi: Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/9819/2024.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**Annania Zachalia Miligo** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 624 DSV** yenye jina la China Road and Bridge Corporation (T) Ltd. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi: Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/9819/2024.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**EDITH DANFORD MACKENZIE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 946 DNA – TOYOTA TOWN ACE.** Chassis namba **KM700012123.** Engine namba **7K0561575.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/24846/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**JACOB MASHARUBU** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 165 DPR – TVS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/218638/2024.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SAIDI ALLY MSOMOKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T620BEV** aina ya **Toyota CRESTA,** Chassis No. **JZX1006095365,** Engine No. **1JZ1083574.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/47244/2024**

# Gachagua amtupia lawama Ruto

**NAIROBI, Kenya**

MAKAMU wa Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, amemshutumu Rais William Ruto kwa ukatili baada ya kuondolewa madarakani na seneti, akieleza kuwa ulinzi wake umeondolewa na maisha yake yanaweza kuwa hatarini.

Akizungumza jana jijini Nairobi baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali ambako alikuwa akipatiwa matibabu kwa maumivu makali ya kifua. Naibu Rais huyo aliyeondolewa madarakani, alimshutumu vikali bosi wake Rais Ruto, akimtuhumu kwa ukatili mkubwa, huku akisisitiza juu ya usalama wake.

Gachagua aliondolewa madarakani na seneti kwa mashtaka matano kati ya 11 yaliyowasilishwa dhidi yake siku chache zilizopita, lakini la agizo la mahakama limesitisha mchakato wa kumteua mrithi wake, ambaye tayari Rais Ruto ameshampendekeza.

"Nimeshtushwa na jinsi mtu niliyemsaidia kuwa rais niliyekuwa na imani naye, na niliyeteswa kwa kumsaidia, alivyoweza kuwa na ukatili mkubwa dhidi yangu," alisema Gachagua.

Aliongeza kuwa, licha ya ulinzi wake kuondolewa, lakini pia na wafanyakazi wake wote wamepewa likizo ya lazima.

"Ikitokea chochote kwangu au kwa familia yangu, Rais William Ruto lazima awajibishwe," alisema, akidai kuwa kumekuwa na majaribio ya awali ya kumuua.

Gachagua aliugua Alhamisi, takriban saa moja kabla ya kutoa ushahidi katika kesi ya kihistoria ya siku mbili ya kumng'oa madarakani. Licha ya kwamba baraza la juu la bunge liliendelea na upigaji kura wa kumwondoa ofisini baada ya mawakili wake kushindwa kuahirisha kikao hicho.

Alipatikana na hatia kwa mashtaka ikiwa ni pamoja na kutishia majaji na kueneza siasa za mgawanyiko wa kikabila, lakini alisafishwa kwenye mashtaka ya ufisadi na utakatishaji fedha.

Katika sakata hilo la kisiasa linalobadilika kwa kasi, Ruto alimteua mara moja Waziri wa Mambo ya Ndani, Kithure Kindiki, kuchukua nafasi ya Gachagua.

Hata hivyo, Mahakama Kuu ilisitisha mchakato wa uteuzi huo dakika chache baada ya bunge kupiga kura kwa wingi kumwidhinisha Kindiki, msomi mwenye umri wa miaka 52 aliyebadilika na kuwa kiongozi mashuhuri wa kisiasa,


huku jopo la majaji watatu likisubiri kusikiliza kesi hiyo leo.

"Rais kwa kukiuka kabisa agizo la mahakama, ameondoa ulinzi wangu kwa ukatili, licha ya bado kuwa makamu wa rais. Sielewi ukatili wa aina hii... wakati mtu akiwa kwenye hali ya chini kabisa maishani na akijitahidi kwa kila hali kuendelea kuishi, unamfanyia ukatili mkubwa kama huo," alisema Gachagua.

Wakati hayo yakiendelea ilielezwa kuwa Rais Ruto bado hajatoa tamko lolote hadharani kuhusu kumwondoa Naibu wake Gachagua madarakani.

Gachagua ni makamu wa rais wa kwanza kuondolewa madarakani kwa njia hii tangu kuanzishwa kwa sheria ya kumwondoa madarakani katika katiba mpya ya Kenya ya mwaka 2010.

*DW*



Mgombea wa kiti cha urais nchini Marekani, Donald Trump, akizungumza katika mkutano huko Pennsylvania jana, alisema anafikiria wagombea wote wa urais wanapaswa kupewa mtihani wa uelewa, huku akisisitiza kwamba yuko sawa kiafya ya akili na mwafaka wa kuingia madarakani. **PICHA: MTANDAO**

# Marekani kuchunguza mpango wa Israel kuishambulia Iran

**WASHINGTON, Marekani**

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Mike Johnson, amesema Marekani inachunguza uvujaji wa nyaraka za siri zinazoelezea tathmini ya Marekani kuhusu mipango ya Israel kuishambulia Iran.

Ilielezwa kuwa nyaraka hizo zilidaiwa kuchapishwa mtandaoni wiki iliyopita na zinasemekana kuelezea picha za satelaiti zinazoonyesha Israel ikihamisha zana za kijeshi kwa ajili ya kujiandaa kukabiliana na shambulio la kombora la Iran la Oktoba 1, mwaka huu.

Pia ilielezwa kuwa nyaraka hizo, ambazo ni siri kuu, zinaweza kusambazwa ndani ya muungano wa mashirika ya kijasusi wa 'Five Eyes' wa Marekani, Uingereza, Kanada, New Zealand na Australia.

Kwa wiki kadhaa Israel imekuwa ikiamua jinsi na wakati wa kujibu shambulio la hivi punde la kombora la Iran. Huku Waziri wa Ulinzi wa Israel akihadharisha kuwa litakuwa kali, sahihi na la kushangaza.

Nyaraka hizo mbili zinaripotiwa kuhusishwa na Shirika la Kitaifa la Ujasusi la Geospatial la Marekani na Shirika la Usalama wa Taifa (NSA), zilichapishwa kwenye akaunti ya Telegram inayofungamana na Iran siku ya Ijumaa.

Johnson, mwanachama wa ngazi ya juu zaidi wa Congress, aliiambia CNN Jumapili kwamba uvujaji huo unatia wasi wasi "Kuna madai mazito yanayotolewa, uchunguzi unaendelea, na nitapata maelezo mafupi juu ya hilo baada ya saa chache," mjumbe huyo wa Republican wa Louisiana alisema.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Pentagon ilithibitisha katika taarifa yake kwamba inafahamu ripoti kuhusu hati hizo, lakini haikutoa maoni zaidi.

Vile vile, mashirika ya Marekani yanayohusika, pamoja na serikali ya Israel, hazijatoa maoni yao hadharani kuhusu uvujaji huo, na kwamba CNN na Axios ziliripoti uvujaji huo, ambao unathibitisha kwa mara nyingine tena kuwa Marekani inamchunguza mshirika wake wa karibu Israel.

Hati moja inarejelea uwezo wa nyuklia wa Israel, ambayo Marekani na Israel kamwe hawajakiri rasmi na kufuatilia mbali matumizi ya chaguo kama hilo katika shambulio lolote lililopangwa.

Ofisa mmoja wa zamani wa ujasusi wa Marekani aliiambia BBC kuwa kutolewa bila kibali kwa hati hizo pengine ni jaribio la kufichua ukubwa wa ulipizaji kisasi uliopangwa, kwa lengo la kuuvuruga.

Maofisa waliambia Associated Press (AP) kwamba Marekani inachunguza iwapo taarifa hizo zilifichuliwa kimakusudi na ajenti wa Marekani, au iwapo ziliibwa, pengine kwa njia ya udukuzi. Nyaraka hizo mbili zinaonekana kutegemea taarifa za satelaiti zilizopatikana kuanzia Oktoba 15 na 16, mwaka huu.

*BBC*

## Ugonjwa wa malaria watokomezwa Misri

**CAIRO, Misri**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema taifa la Misri limefanikiwa kutokomeza kabisa ugonjwa wa malaria unaoenezwa na kimelea cha plasmodium kinachotokana na mbu jike aina ya Anofelesi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa WHO, Tedros Ghebreyesus juzi, matokeo hayo ya kihistoria, ni kilele cha karne ya juhudi za kutokomeza malaria, ugonjwa hatari unaoweza kuua binadamu.

Ghebreyesus alisema malaria ni ugonjwa wa zamani nchini Misri, lakini kwa sasa umekuwa ni ugonjwa wa kihistoria na sio mustakabali wa taifa hilo tena.

"Kuidhinishwa kwa Misri kama nchi isiyo na malaria ni tukio la kihistoria kweli na inaonyesha dhamira ya watu wa Misri na serikali ya kujikwamua na janga hili la kale," alisema Ghebreyesus.

Ilielezwa kuwa uthibitisho wa kutokomeza malaria unatolewa na WHO wakati nchi hiyo imethibitisha kwamba mlolongo wa maambukizi ya ugonjwa huo na mbu umekatizwa katika ngazi ya kitaifa kwa angalau miaka mitatu iliyopita. Na kwamba ulimwenguni, nchi 44 zimethibitishwa kuwa hazina malaria.

Kwa mujibu wa WHO, malaria inaua zaidi ya watu 600,000 kila mwaka, na asilimia 95 kati yao wakiwa barani Afrika.

Hata hivyo, ikiwa bara linachangia asilimia 94 ya visa vya ugonjwa huo, nchi tano za Afrika zinaonekana kwenye orodha hiyo ikiwamo Algeria, Cape Verde, Lesotho, Mauritius na Ushelisheli.

Kwa upande mwingine, asilimia 70 ya mzigo wa malaria duniani unaangukia nchi 11 za Afrika ikiwamo Burkina Faso, Cameroon, Ghana, Mali, Msumbiji, Niger, Nigeria, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudani na Tanzania.

*RFI*

**"Kuidhinishwa kwa Misri kama nchi isiyo na malaria ni tukio la kihistoria kweli na inaonyesha dhamira ya watu wa Misri na serikali ya kujikwamua na janga hili la kale," alisema Ghebreyesus.**

# TABORA UNITED YATIMUA KOCHA WA SITA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United imemtimua kocha wake mkuu, Frances Kimanzi raia wa Kenya, siku chake baada ya kupokea kipigo cha mabao 4-2 kutoka kwa JKT Tanzania.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo, imesema imeamua kufikia makubaliano ya kuachana na kusitisha mkataba naye kwa makubaliano ya pande mbili.

"Uongozi wa Tabora United unapenda kuutaarifu umma kuwa imefikia makubaliano ya pande mbili kusitisha makubaliano baina ya yaliyekuwa Kocha Mkuu, Francis Kimanzo pamoja na msaidizi wake, Yusuph Chippo kuanzia leo Oktoba 21.

"Sababu za kusitisha makubaliano hayo ni kutokana na mwenendo usioridhisha na matokeo ambayo timu imekuwa ikiyapata.

Uongozi unawashukuru kwa kipindi chote walichokuwa nasi katika utumishi wao na tunawatakiwa kila la heri kwenye maisha yao nje ya Tabora United," ilieleza taarifa hiyo iliyotolewa na Ofisa Habari wa klabu hiyo kwa niaba ya mtendaji mkuu.

Ijumaa iliyopita, Tabora United ilichapwa mabao 3-2 dhidi ya JKT Tanzania, mchezo uliochezwa, Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam, ukiibakisha timu hiyo kwenye nafasi ya 11 na pointi nane.

Kocha huyo ameiongoza Tabora United michezo minane, ikishinda mawili, sare mbili na kupoteza minne.

Kabla hata dirisha dogo la usajili halijafika, tayari jumla ya makocha sita kati ya 16 hawapo kwenye timu zao kutokana na kufanya vibaya, watano wakiwa ni wa kigeni.

Kocha wa kwanza alikuwa ni David Ouma wa Coastal Union, raia wa Kenya, ambaye alitimuliwa kabla hata ligi haijaanza kwa kile kilichodaiwa kufanya vibaya kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Msenegal Youssouph Dabo wa Azam FC, Fikiri Elias wa KenGold, Mserbia, Goran Copunovic wa Pamba Jiji na Paul Nkata wa Kagera Sugar, raia wa Uganda.

## KAMA RASHFORD!...



Vijana wakicheza mpira katika uwanja wa mchanga wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana huku anayepiga mpira akifananishwa na mshambuliaji wa Manchester United ya England, Marcus Rashford. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zahera naye alia Namungo kunyimwa penalti

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo, Mwinyi Zahera, amemlalamikia mwamuzi, Aboubakar Mturo kutoka Mtwara, kuwanyima penalti dhahiri na kuwapa wapinzani wao Singida Black Stars, kitu ambacho kimesababisha kupoteza mechi kwa mabao 2-0 juzi kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Zahera, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ameshangaa aina ya penalti aliyowapa Singida, wakati hata wao mchezaji wao aliwekwa mguu ndani ya eneo la hatari.

Lawama hizi zimekuja siku chache tu baada ya mchezo wa dabi, Simba na Yanga uliochezwa Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambapo mwamuzi Ramadhani Kayoko, alishindwa kutoa japo tuta moja wakati winga, Kibu Denis alipofanyiwa madhambi mara mbili na wachezaji wa Yanga ndani ya eneo la hatari.

"Kipindi cha kwanza walitushambulia sana na kusababisha tuwe tunashuka chini, kipindi cha pili tulifunguka, lakini wenzetu walipata nafasi ya kufunga, tulinyimwa penalti dhahiri, lakini kwao ikawa penalti, inashangaza sana," alilalamika kocha huyo.

"Mchezaji Antony Mlingo alionekana kuwekewa mguu na mchezaji mmoja wa Singida, lakini mwamuzi alipeta, baadaye Abdoulaye Yonta Camara, aliangushwa ndani ya eneo la hatari na Khamis Khalifa na mwamuzi akaamuru penalti iliyowekwa nyavuni na Marouf Tchakei aliyepachika mabao yote mawili kwenye mchezo huo.

Kocha Mkuu wa Singida, Patrick Aussems, aliwashangaa Namungo kwa jinsi wanavyocheza haifanani na nafasi waliopo.

"Nafikiri walikuja hapa kuchukua pointi moja, walicheza zaidi nyuma ya mpira, tukapata shida sana kuwafungua kwa sababu tulikuwa hatushambulii tukiwa na idadi kubwa ya watu eneo la mpinzani, kipindi cha pili tukabadili mfumo, tukawafungua kwa kushambulia pembeni na pasi mpenyezo, tukafunga mabao mawili, ingekuwa zaidi ya hayo kwani tulipata nafasi nyingi, Namungo ni timu nzuri, nafasi waliyonayo kwenye msimamo haifanani na wanachokitoa uwanjani," alisema.

Singida bado imeendelea kung'ang'ania kileleni ikiwa na pointi 19 kwa michezo saba iliyocheza, ikishinda sita na sare moja, huku Namungo ikiwa nafasi ya 13 na pointi zake sita.

## Zimamoto yaifungua mdomo Uhamiaji FC

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

USHINDI wa mabao 2-1, iliyoupata Uhamiaji FC juzi dhidi ya Zimamoto FC kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu Zanzibar, umeipa nafasi ya kutamba kwa kudai kwamba siri ya mafanikio hayo ni maboresho yao waliyoyafanya.

Katika mchezo huo wa raundi ya saba uliopigwa Uwanja wa New Amaan Complex juzi na Uhamiaji kuibuka na ushindi, unaifanya timu hiyo kufikisha alama 13 na kujiweka nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu wakati Zimamoto SC wakisalia nafasi ya 11 na alama zao nane.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Abdul-saleh Abdallah, alisema miongoni mwa maboresho waliyofanya ni katika safu ya ulinzi ambayo haikuwa vizuri na kuruhusu mashambulizi ya mara kwa mara kwenye mechi zilizopita.

Alisema safu yake ya ulinzi mara kwa mara inakatika na kusababisha hata wanapopata bao hurudishwa muda mchache.

"Kupitia mchezo huo benchi la ufundi kwa ujumla tumeona mabadiliko kwa wachezaji wa safu hiyo, wamecheza vizuri ingawa kuna wakati walikuwa wakipoteana tulipokuwa tunashambuliwa," alisema.

## Wavu Taifa Cup kupigwa Dodoma

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Taifa Cup ya mchezo wa wavu, yanatarajiwa kutimua vumbi jijini Dodoma kuanzia Desemba 2-8, mwaka huu, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wavu Tanzania (TAVA), Shukuru Ally, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu kutoka mikoa ya Tanzania Bara pamoja na visiwani Zanzibar.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kuwapa fursa vijana kuonesha vipaji vyao pamoja na kuuinua mchezo huo mikoani.

"Viongozi wa mikoa wajitahidi kuhimiza viongozi wa timu wathibitishe kushiriki mashindano hayo kwani timu inaposhiriki inautangaza mkoa husika," alisema Ally.

Katibu huyo alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vema kwani na kwamba kwa upande wa visiwani Zanzibar tayari wametumiwa barua ili kuthibitisha ushiriki wao.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHUKWUEZE NA EVERTON
KLABU ya Everton inapanga kumsajili winga wa AC Milan kutoka Nigeria, Samuel Chukwueze mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

### DAVIES KUSHAWISHIWA
KLABU ya Manchester United inalenga kumshawishi beki wa pembeni wa Bayern Munich, Alphonso Davies, 23. ***(Fichaje)***

### VLAHOVIC ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inaweza kumpata Mserbia Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 24, baada ya kumsaka kwa muda mrefu kwa bei nafuu kwa sababu mazungumzo ya mshambuliaji huyo wa Juventus na klabu yake kuhusu mkataba mpya hayaendelei vizuri. ***(Caught Offside)***

### TUCHEL AMTENGA LOW
KOCHA mpya wa England, Thomas Tuchel ametengana na mshirika wake wa muda mrefu wa ukufunzi Zsolt Low. (Sun)

### MBEUMO AWINDWA VILLA
KLABU ya Aston Villa imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Cameroon, Bryan Mbeumo mwenye umri wa miaka 25, kutoka Brentford. ***(TBR Football)***

### ZIRKZEE KUACHIWA
KLABU ya Manchester United huenda ikamwachilia kwa mkopo mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23, kwa Juventus ikiwa watamsajili mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia Benjamin Sesko mwenye miaka 21, msimu ujao. ***(Tuttomercato)***

### MORO AGOMBEWA
KLABU za Manchester City, Liverpool na Tottenham Hotspur, zimeelekeza macho yao kwa winga wa Real Valladolid, Mhispania Raul Moro, 21. ***(Fichajes)***

### JAMIE KWA SPURS, ARSENAL
NYOTA wa England, Jamie Bynoe-Gitten mwenye miaka 20, amezivutia Arsenal, Tottenham, Crystal Palace na Nottingham Forest - ingawa klabu hiyo ya Ujerumani inataka zaidi ya pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo kabla ya kufikiria kumuuza. ***(Caught Offside)***

### PAZ ANYATIWA JUVE
KLABU za Arsenal, Juventus, AC Milan na Napoli ni miongoni mwa zinazomtazama kiungo wa kati wa Como na Argentina, Nico Paz, 20. ***(Nicolo Schira on X)***

### MARMOUSH AWANIWA LIVER
LIVERPOOL inavutiwa na mshambuliaji wa Eintacht Frankfurt na Misri, Omar Marmoush mwenye umri wa miaka 25. Nottingham Forest na Aston Villa zilitaka kumsajili msimu uliopita. ***(Sky Germany)***

### BEI YA KUDUS
KLABU ya West Ham inatarajiwa kutoa bei ya kiungo wao wa kati kutoka Ghana Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 24. Liverpool, Arsenal, Manchester City na Chelsea zimeonesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI APIGA HAT-TRICK NDANI YA DAKIKA 11 TU

## ●●●Aingia katika mbio za kuwania kiatu cha dhahabu pamoja na Suarez na Benteke wa...

**MIAMI, Marekani**

LIONEL Messi alifunga hat-trick ya kushangaza ndani ya dakika 11 kuisaidia Inter Miami kuvunja rekodi ya kuwa na alama nyingi katika msimu mmoja, baada ya kuishinda New England mabao 6-2 kwenye Uwanja wa Chase huko Fort Lauderdale, Florida.

Miami alihitimisha msimu wa Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), na alama 74 katika michezo 34.

Luis Suarez alianza kwa kufunga mabao mawili kabla ya Messi ambaye ni mshindi mara nane wa Ballon d'Or kufunga hat-trick.

Miami pia ilikuwa timu ya kwanza katika historia ya MLS kuwa na wachezaji wengi wenye angalau mabao 20 kwa msimu.

Kwa mabao 20, Messi na Suarez wanawania kiatu cha dhahabu pamoja na Christian Benteke wa DC United.

"Nahodha wetu ametuongoza, wachezaji wametuongoza katika nyakati ambazo ilikuwa ngumu," alisema mmiliki mwenza wa Miami, David Beckham.

# Slot atoa la moyoni kuhusu waamuzi

**LIVERPOOL, England**

ARNE Slot amesema mwamuzi John Brooks, alitaka kuthibitisha kwamba hatishwi na umati wa Anfield wakati Liverpool iliposhinda mabao 2-1 dhidi ya Chelsea.

Mchezo wa Jumapili ulionesha ukaguzi kadhaa wa VAR ikiwa ni pamoja na tukio la dakika ya sita ambapo Tosin Adarabioyo alioneshwa kadi ya njano kwa kumvuta Diogo Jota.

Liverpool walipata bao la uongozi kupitia Mohamed Salah aliyefunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 29, iliyotolewa baada ya Levi Colwill kumgonga Curtis Jones.

Nicolas Jackson aliisawazishia Chelsea dakika ya 48 - bao ambalo lilichukuliwa kuwa la kuotea uwanjani, lakini likapinduliwa baada ya ukaguzi wa VAR - kabla ya Salah kufunga bao la ushindi dakika ya 51.

Liverpool walisubiri kupata ushindi ambao uliwarejesha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, lakini Slot alipendekeza wangefurahia alasiri ya starehe ikiwa maafisa wangechukua mbinu tofauti.

Alipoulizwa kuhusu hali ya Anfield, bosi huyo wa zamani wa Feyenoord alisema: "Mashabiki walikuwa muhimu sana kwetu. Sijui kama hili ni jambo ambalo watu wanasema Uingereza, lakini walisema katika klabu yangu ya zamani, ambayo pia ilikuwa uwanja wa kuvutia, kwamba 'ndiyo, waamuzi wanavutiwa kidogo na umati na ndiyo maana unapata maamuzi rahisi kwa niaba yako.'

"Lakini leo (juzi) ilionesha haijalishi mashabiki walikuwa na kelele kiasi gani, mwamuzi alitaka tu kuonesha kuwa hawezi kutoa maamuzi aliyopaswa kufanya. Kwa hiyo haikutusaidia kwa mwamuzi, lakini hakika iliwasaidia wachezaji wetu kwa sababu wao ilibidi kufanya kazi kwa bidii sana.

"Ikiwa kila wakati wanashangilia sana kwa ajili yako ikiwa unapiga mpira wa kuzuia, au Darwin Nunez akarudi nyuma, au dakika hizi zote, hakika inakusaidia kiakili. Walikuwa muhimu sana kwa wachezaji, lakini kwa bahati mbaya, haikuwa hivyo.

Slot alielezea ushindi wa Jumapili dhidi ya Chelsea kama mgumu zaidi katika kipindi chake hadi sasa.

## Guardiola: City haijazoea kushinda 'jioni'

**MANCHESTER, England**

BAO la ushindi la dakika za mwisho la Manchester City dhidi ya Wolves kwenye Ligi Kuu England Jumapili liliamuliwa kwa usahihi na lilistahili zawadi kwa uvumilivu wa wachezaji wake, kocha Pep Guardiola alisema.

Huku City wakionekana kuelekea kwenye sare ya 1-1 licha ya kumiliki mpira kwa kiasi kikubwa, John Stones alifunga kwa kichwa dakika ya 95.

Kiungo wa kati wa City Bernardo Silva alikuwa karibu na Sa, lakini Mwamuzi Msaidizi wa Video (VAR), aliona kuwa hakuzuia mtazamo na Kavanagh akabatilisha uamuzi wake.

"Bernardo hasumbui nafasi ... Sa alikuwa na maono mazuri. Mfungaji kutoka kwa Phil [Foden] na mpira wa kichwa ulikuwa mzuri," alisema Guardiola, ambaye alisherehekea ushindi wa mabao 2-1 ambao uliiweka City kileleni kwa muda mfupi hadi Liverpool walipopata ushindi kama huo dhidi ya Chelsea.


"Hatujazoea kushinda mechi mwishoni, kama (kocha wa zamani), Jurgen Klopp akiwa Liverpool ambapo ilifanyika mara nyingi. Ni ladha nzuri kwetu," Guardiola aliongeza.

City walikuwa na asilimia 78 ya kumiliki mpira dhidi ya timu ya Wolves inayopigania maisha yao chini kabisa ya jedwali.

"Kukiwa na wachezaji 11 kwenye nafasi ya penalti, ni ngumu sana," Guardiola alisema, akikumbuka kwamba timu yake ilipoteza huko Molineux msimu uliopita. "Lakini tulikuwa na subira ... Sisi ni nani na hiyo ni nzuri sana."

Hata hivyo, alikuwa na huruma kwa wapinzani wake. "Tumekuwa katika nafasi hiyo, unapopoteza mwisho. Lakini huu ndio mchezo.

"Tulicheza jinsi tunavyotaka kucheza na ni furaha kuwa hapa, kufunga katika sekunde 50 za mwisho na kwenda kileleni mwa ligi."



## FLICK ASHANGAA MAPOKEZI YA GAVI BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, amesema mapokezi aliyopewa Gavi yalimshtua baada ya kiungo huyo kurejea kutoka chumba cha majeruhi ambapo alikuwa nje ya dimba kwa miezi 11 na kurudi wakati wa ushindi wa 5-1 dhidi ya Sevilla Jumapili kwenye LaLiga.

Gavi hakucheza tangu alipoumia misuli ya paja alipokuwa akiichezea Hispania Novemba mwaka jana, lakini aliingia akitokea benchi kwa dakika 10 za mwisho dhidi ya Sevilla kwenye Uwanja wa Olympic.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alichukua nafasi ya Pedri, akichukua kitambaa cha unahodha na alishangiliwa sana alipoingia uwanjani na mashabiki wa Barca.

"Nimefurahia matokeo haya na haswa kwa Gavi," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari.

"Inashangaza sana unapoona hali ya hewa uwanjani na mashabiki. Ilikuwa na napenda hii."

Mashaka yoyote kuhusu iwapo uchezaji mkali wa Gavi ungeathiriwa na jeraha lake yaliondolewa haraka alipokuwa akiingia kwenye changamoto hiyo.

"Nguvu aliyotoa kwenye mechi alipoingia ilikuwa nzuri," aliongeza Flick.

"Lakini ni kawaida, ni njia yake ya kucheza. Wakati mwingine ni sawa kuwa mtulivu zaidi, lakini si mtindo wake wa uchezaji."

Gavi alisema amefurahi kurejea, aliwashukuru wachezaji wenzake na mashabiki kwa sapoti yao na kusema muda wake nje umemsaidia kufahamu jinsi alivyo na bahati.

"Nimekuwa nikiota juu ya hili kwa miezi mingi na ninashukuru kwa wachezaji wenzangu ambao walinirahisishia mchakato.

"Kitu kigumu zaidi si kucheza, kutazama kutoka nje. Inakatisha tamaa, ni ngumu. Lazima ufurahie kila wakati na [muda wa kuisha] hukuruhusu kuthamini vitu ulivyo navyo. Najihisi mwenye bahati kurejea.

"Nilikosa kucheza mpira zaidi, haya ni maisha yangu, ndivyo nimekuwa nikifanya. Wakati mashabiki wote na wachezaji wenzako wanakupenda na kukupa mapokezi hayo, unajisikia bahati sana."

HABARI MICHEZO

# TUZO ZA TFF ZAWAPA KIBURI FOUNTAIN GATE

Na Adam Fungamwangwo

BAADA ya kutangazwa kuwa Kocha Bora wa Septemba, Mohamed Muya wa Fountain Gate, ameibuka na kusema ataendeleza ubora wake ili kuifanya timu anayoifundisha kuwa bora zaidi na tishio kwa ajili ya kupata tuzo nyingi zaidi, huku timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya KMC jana kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati mkoani Manyara.

Akizungumza kutoka mkoani humo, Muya ambaye alitangazwa hivi majuzi kuwa kocha bora wa mwezi huo, akiwashinda Rachid Taoussi wa Azam FC na Denis Kitambi wa Singida Black Stars, amesema anajisikia faraja huku akisema si tuzo yake pekee bali ni ya klabu nzima, akimpongeza pia mchezaji wake, Selemani Mwalimu kuwa mchezaji bora wa mwezi huo.

"Ni jambo kubwa sana kwangu mimi na klabu yetu, tuzo nimepata mimi, lakini kazi imefanywa na watu wengi, ndiyo maana utaona hata kile nilichokuwa naelekeza wachezaji kimesababisha straika wangu, Selemani Mwalimu naye kupata tuzo, nampongeza sana, nadhani hii imetupa chachu ya kuendelea kujituma zaidi na zaidi ili tuweze kupata mafanikio, tutapambana ili kuendelea kuzoa tuzo nyingi zaidi zitakazoifanya pia timu yetu izidi kuwa tishio kwenye Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Naye Ofisa Habari wa klabu hiyo, Issa Mbuzi, amesema tuzo tatu walizozipata zinaonesha kabisa kuwa Fountain Gate ni moja kati ya timu tishio nchini, akizionya timu zingine za Ligi Kuu kuwa msimu huu wana lao jambo.

"Hapo ndipo timu zijue kuwa tuna kikosi cha aina gani, tuna mchezaji bora, kocha bora wa mwezi na mchezaji ambaye aliingia fainali na itacheza kwenye uwanja ambao meneja wake naye ametwaa tuzo," alitamba Ofisa Habari huyo.

Mwalimu alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mwezi baada ya kuwashinda Feisal Salum wa Azam FC na mchezaji Edgar William pia wa Fountain Gate ambao waliingia nao fainali katika mchakato huo, huku Kamati ya Tuzo ya TFF ikimtangaza Meneja wa uwanja huo, Godwin Israel kuwa meneja bora wa mwezi huo.

Katika mchezo wa jana, straika huyo aliongeza bao lingine, akifikisha mabao sita akizidi kuwa juu ya kilele cha ufungaji bora, huku Edgar akifikisha bao la nne, lingine likifungwa na Dickson Ambundo ambaye sasa ana mawili, huku la kufutia machozi kwa KMC likifungwa na Andr



MAGONGO...

Watoto wakijifunza kucheza mpira wa magongo katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mpole afungua akaunti ya mabao

Na Adam Fungamwangwo

MSHINDI wa Kiatu cha Dhahabu Tanzania Bara msimu wa 2021/22, George Mpole, amefungua akaunti yake ya mabao msimu huu, akifunga bao la kwanza akiwa na timu yake ya Pamba Jiji FC ambayo imeendelea kusotea ushindi wa kwanza wa Ligi Kuu hadi kufikia mchezo wa nane.

Mpole, aliyefunga mabao 17 msimu wa 2021/22, akimzidi bao moja aliyekuwa mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, na baada ya hapo akatimkia St Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, juzi alifunga bao la kusawazisha dakika ya 75, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, akiinusuru timu yake kwa kipigo kutoka kwa Kagera Sugar.

Kabla ya kufunga bao hilo, Peter Lwasa alikuwa ameifungia bao Kagera Sugar dakika ya 44, na dakika 90 zikaisha timu hizo zikiwa sare ya bao 1-1.

Sare hiyo, inaendelea kuifanya Pamba Jiji kuwa timu pekee ya Ligi Kuu ambayo haijashinda mchezo wowote msimu huu, ikiwa imefikisha michezo minane. Timu hiyo ambayo imecheza michezo minane, imetoka sare tano na kupoteza michezo mitatu ikiwa nafasi ya 15, ikikusanya pointi tano tu mpaka sasa.

Pamba Jiji ni miongoni kwa timu tano ambazo zimefukuza makocha wao mpaka sasa, baada ya kumfuta kazi Goran Copunovic, na hivi karibuni imemtangaza kocha Fred Felix Minziro ambaye ni mchezo wake wa kwanza baada ya kuwa kocha akianza na sare.

Wakati huo huo, Klabu ya Kagera Sugar imemtangaza kocha Melis Medo kuwa Kocha Mkuu, akiisimamia timu hiyo kwa mara ya kwanza, akitokea Mtibwa Sugar.

Hivi majuzi alitangazwa kuwa kocha bora wa Septemba, akiwa na kikosi hicho kinachopambana kwenye Ligi ya Championship ili kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

## Gamondi aihofia JKT, Fadlu sasa ataka VAR

INATOKA UK. 24

fanyika sahihi.

"Tulinyimwa penalti mbili na mchezaji mmoja wa Yanga alipaswa kupewa kadi nyekundu kwenye mchezo uliopita, Ligi ya Tanzania kubwa kama hii sasa inahitaji VAR, itafanya mpira wa nchini kukua kwani kutakuwa na maamuzi sahihi na kila mmoja atapata anachostahili, kama si mechi zote hata kwenye michezo mikubwa, nchi nyingi za Afrika sasa zinatumia na imeleta athari chanya," alisema kocha huyo.

Nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein „Tshabalala', amesema wanatambua kuwa huwa wanapata tabu sana wanapocheza dhidi ya Prisons kwenye uwanja huo, lakini safari hii watahakikisha hawaruhusu bao.

Msimu uliopita, Simba ililala mabao 2-1 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye uwanja huo.

"Tumekuwa na matokeo magumu sana tukiwa hapa Mbeya, hilo tunalijua na tumekuja kupambana na jukumu la kwanza ni kuhakikisha haturuhusu bao," alisema.

Mbwana Makata, Kocha Mkuu wa Prisons, alikubali muziki wa Simba, akisema waliiona ikicheza dhidi ya Yanga, hivyo wataingia kwa tahadhari.

"Maandalizi ni mzuri, tunawaheshimu ni moja ya timu nzuri na hata mchezo dhidi ya Yanga walicheza vizuri mno, walikuwa wanacheza na kubadilika, wana wachezaji wenye uzoefu kwa hilo tunawaheshimu, kwa maana hiyo tumetengeneza mpango mkakati mbele ya timu iliyokuwa bora," alisema.

Simba ina pointi 13, ikiwa kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu, ikicheza michezo sita, Prisons ikishika nafasi ya 12, ikikusanya pointi saba kwa mechi saba ambazo imecheza mpaka sasa.

## TFF yazishukia Simba, Yanga

INATOKA UK. 24

wa TFF.


Mfungaji wa bao la kwanza, Mashaka alisema alicheza mchezo huo akiwa majeruhi, lakini alikubali kuingia dimbani kwa sababu ya uzalendo.

"Nilicheza nikiwa na majeraha, ilikuwa nisicheze, lakini nikaona hii ni mechi yangu kwa majeraha haya niliyokuwa nayo bado naweza kuingia uwanjani kulipambania taifa, ndiyo maana uliona nilicheza nikapambana nikafunga bao, pale nilipozidiwa nilitolewa na akaingia mtu mwingine," alisema.

Naye Shekhan, alisema amefurahi kufunga bao la pili na la ushindi, akisema awali walianza vibaya michuano hiyo kwa sababu hawakuwa wanaelewana kutokana na kila mchezaji kutoka kwenye timu tofauti.

Tanzania na Kenya, zote zimefuzu kucheza fainali za AFCON chini ya miaka 20 zitakazofanyika mwakani kwenye nchi ambayo itatangazwa baadaye.

**Messi apiga hat-trick ndani ya dakika 11**
UKURASA 21



Michezo
Jumanne Oktoba 22, 2024
Nipashe

**MSITUNI!...**



Mshambuliaji wa Chelsea, Nicolas Jackson, akipambana kuwania mpira katikati ya msitu wa mabeki wa Liverpool kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Anfield na Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI AIHOFIA JKT, FADLU SASA ATAKA VAR

## Asema wamekuwa waathirika kwa waamuzi, ni wakati Simba, Yanga zikishuka tena uwanjani leo kusaka...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumaliza dabi yao Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga leo watashuka tena dimbani kucheza mechi zao za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, wakati Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi akisema haoni kama timu yake inaweza kushinda idadi kubwa ya mabao leo itakapocheza dhidi ya JKT Tanzania saa 1:00 usiku, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, wa Simba Fadlu Davids, amesema wamekwenda Mbeya kusaka pointi tatu ili kukaa kwenye reli ya kusaka ubingwa, ambapo watashuka, Uwanja wa Sokoine, saa 10:00 jioni kucheza dhidi ya Prisons, akiwatahadharisha waamuzi kuchezesha kwa haki, akitaka pia VAR itumike kwenye michezo ya ligi.

"Nafikiri hatuwezi kushinda mabao mengi katika mchezo huu, ikumbukwe hawa msimu uliopita tulitoka nao sare.

"Nimeiangalia timu hii, ina uwiano mzuri wa kushinda ikicheza nyumbani, imepoteza mchezo mmoja tu, ikionekana ni ngumu kufungika na mabeki wake wako vizuri, hivyo tumelifanyia kazi, tunahitaji kupambana ili kushinda tena mchezo, nafikiri itakuwa mechi ngumu inabidi tuwe makini, hawa jamaa mashambulizi yao wanaanzia nyuma na wanapenda kushambulia pembeni na pasi ndefu pia," alisema Gamondi.

JKT Tanzania inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, ikicheza michezo saba, ikishinda miwili, sare nne, ikipoteza mchezo mmoja.

Yanga ambayo itaingia uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kuwachapa watani zao wa jadi bao 1-0 Jumamosi iliyopita, itacheza mchezo wake wa sita wa ligi, ikiwa nafasi ya pili, imeshinda mechi zote tano, ikiwa ni timu pekee ambayo wavu wake haujaguswa mpaka sasa.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, amekiri kuwa anakwenda kucheza mchezo mgumu dhidi ya Yanga.

"Ni timu bora kwa sasa hapa nchini, na inaleta ugumu hata kwa baadhi ya timu nje ya nchi, ukiangalia hata mchezo uliopita dhidi ya Simba, aliwatoa kina Pacome Zouzoua, Prince Dube, na Stephane Aziz Ki, lakini aliingiza wachezaji ambao walikwenda kubadili mchezo, hivyo kazi yetu kubwa itakuwa kwenye kuuzuia na kupambana na ubora wao, kwa bahati nzuri ninao aina ya wachezaji hao," alisema kocha huyo.

Fadlu, Kocha Mkuu wa Simba amesema timu yake imejipanga vema, licha ya kucheza mechi ngumu dhidi ya Yanga kwenye uwanja uliokuwa unateleza kutokana na mvua, lakini haijalishi badala yake wamekwenda kuchukua pointi tatu, huku akiiomba mamlaka ya soka nchini kuwa na VAR kwenye Ligi Kuu kwani wamekuwa waathirika wa makosa ya waamuzi.

"Tulicheza mchezo mgumu dhidi ya Yanga, tumepumzika siku mbili tu pamoja na kusafiri, tuna kazi ya kufanya, tunaiheshimu Prisons lakini tumekuja Mbeya kuchukua pointi tatu, hili litawezekana kama maamuzi yata-

INAENDELEA UK. 23

# TFF yazishukia Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, amezitaka timu za Ligi Kuu zenye wachezaji walio chini ya miaka 20 na hawapati nafasi za kucheza dakika nyingi, watolewe kwa mkopo kwenye timu zingine zenye mahitaji.

Rais huyo alisema hayo baada ya kumalizika kwa michuano ya Afrika Mashariki na Kati, Ukanda wa CECAFA, ikishuhudiwa Timu ya Taifa ya Tanzania, Ngorongoro Heroes, ikitwaa ubingwa kwa kuifunga Kenya mabao 2-1, katika mchezo wa fainali uliochezwa juzi, Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam.

Mabao ya washindi yalifungwa na Valentino Mashaka ambaye ni straika wa Simba, na Shekhan Khamisi anayeitumikia Yanga katika nafasi ya kiungo, wote wakiwa hawapati nafasi mara kwa mara katika vikosi vya kwanza vya timu hizo.

Karia alisema wachezaji hao vijana wanapaswa kupata dakika nyingi za kucheza ili wawe bora, wainue viwango vyao na kuwa na utayari kimwili.

"Tunaendelea kuzitunza timu zote za taifa chini ya miaka 17 na 20, na wale wachezaji ambao wapo kwenye timu mbalimbali za Ligi Kuu ambao hawapati nafasi kwenye vikosi vyao, klabu ziwapeleke kwa mkopo kwani zipo ambazo zinahitaji wachezaji, Ligi Kuu na hata Championship," alisema Karia.

Akizungumzia mashindano hayo alisema yalikuwa mazuri na magumu, huku akisifu maandalizi yaliyofanyika.

"Ilikuwa ni michezo mizuri, lakini migumu, Watanzania wamepata burudani pia malengo ya CECAFA yamefikiwa kwa kuandaa na kumaliza salama washindi wakipatikana, sisi kama Watanzania tujipongeze kwa timu yetu kupata nafasi ya kucheza fainali za AFCON kwa vijana 2024/25 na pia kuwa mabingwa, tumerudia historia miaka minne iliyopita nchini Uganda, tulipowafunga Kenya bao 1-0 tukawa mabingwa, nakumbuka wakati huo nahodha alikuwa Dickson Job, Novatus Dismas, Abdul Selemani Sopu na wengineo," alisema rais huyo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >